Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 80 No. 213 | JUM.II-RAJ.1440 AH | MACHI 2020 | AMMAN 1399 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

(Hao ndio) wanaotubu, wanaoabudu, wanaotukuza, wanaofunga saumu, wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamuru yaliyo mema, na wanaozuia yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Allah - na wape habari njema waaminio.
(AT-TAUBA 9:112)

Ujumbe Maalum kutoka kwa Hadhrat Khalifatul Masih V atba

Hadhrat Amirul Mu'minin atba alitoa ujumbe maalum kwa ajili ya Wanajumuiya wote duniani. Kutokana na maagizo ya Serikali ya Uingereza ya kutokuhudhuria msikitini kusali ikiwa ni hatua kujihadhari na ugonjwa wa virusi vya Corona (Covid-19), Huzur Aqdas atba alitoa ujumbe huu akiwa amekaa ofisini kwake iliyoko Tilford, Islamabad.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa ujumbe maalum kwa Waahmadiyya toka ofisini kwake na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Baada ya kusoma Tashahud na Ta'awuz, Hahdrat Khalifatul Masihi wa Tano atba alisema: "Siku hizi kutokana na kuenea kwa ugonjwa wa virusi, Serikali za nchi nyingi zimechukua hatua dhibiti. Hapa Uingereza pia Serikali imepiga marufuku kwamba sala ya jamaa haiwezi kusaliwa msikitini, na kama ikisaliwa idadi isizidi watu wawili au wachache ambao wawe ndugu wa karibu tu.

Kwa sasa sheria bado haijawa wazi. Baadhi wanaeleza kuwa hawa (wanaosali) wawe jamaa wa karibu na wengine wanasema hata marafiki au wale ambao wanakaa pamoja pia wanaweza kushiriki. Kwa hiyo, katika hali kama hii Sala ya Ijumaa haiwezi kusaliwa mpaka ibainike vizuri kwani kuhusiana na Sala ya Ijumaa baadhi ya vipengele pia vinahitaji ufafanuzi zaidi. Ndiyo maana, leo baada ya kushauriana, nimeamua kwamba niongee nanyi nikiwa nimekaa ofisini katika sura ya ujumbe badala ya kutoa hotuba na Sala ya Ijumaa isisaliwe rasmi.

Siku ya Ijumaa wanajumuiya wamezoea kusikiliza hotuba ya Khalifa wa zama. Leo muda huu nisipowahutubia watu huenda watavunjika moyo au badala yake wataanza kuwa na mawazo ya aina nyingi. Kwa hiyo, nimeona ni bora niongee na wanajumuiya kwa namna moja au nyingine na nimetumia njia hii ya kukaa ofisini na kuzungumza nanyi kwa sura ya ujumbe.

Kama nilivyosema, leo hatutasali Sala ya Ijumaa na utaratibu utakaotumika katika siku za baadaye Insha'Allah utatangazwa. Hatuwezi kuacha Sala ya Ijumaa kwa muda mrefu. Ni muhimu kwangu kuwasiliana na wanajumuiya na hususani katika siku hizi ni muhimu mno. Hivyo, Insha'Allah tutatafuta suluhisho la jambo hili baada ya kushauriana na mawakili na watu husika.

Ningewaambia na wanajumuiya pia kuwa kwa sababu Serikali imekataza kuhudhuria msikitini kutokana na ugonjwa huu; au kama haijakataza kwa mfano hapa Uingereza inaruhusiwa kwa mtu mmoja mmoja kufika msikitini na kusali; au wanafamilia wachache pia wanaruhusiwa kusali wakiwa na nafasi kati yao kiasi kwamba wasikaribiane sana. Pamoja na hayo, sala ya jamaa haiwezi

Endelea uk. 2

Upendo wa Seyidna Ahmad as kwa Mtume saw

Na **Sheikh Karim Ud Din Shams Mbeya**



Kwa hakika hatuwezi kueleza upendo wa Seyidna Ahmad as kwa Bwana wake, Mtume Mtukufu saw kwani hatuna maneno yawezayo kubainisha vizuri, mapenzi mahaba na uaminifu wake kwa Mtume saw. Seyidna Ahmad as alimpenda Bwana wake kwa kila namna, upendo wake na Ikhlasi yake kwa Mtume saw haina mipaka, hakuna mtu awezaye kuvieleza na kuvipima kwa kipimo cha aina yoyote.

kwa kifupi tunaweza kusema kuwa, upendo wake kwa Bwana wake ulikuwa kiini cha roho yake na uzima wake, matukio mbali mbali, yapendezayo ya mapenzi na mahaba, yanaonekana maishani mwake kiasi hiki kwamba mtu anapigwa na bumbuwazi.

Masharti na vigezo vyote vya mapenzi ya kweli vina hakiki katika kila secunde ya maisha yake, ambayo yananga'a na mifano ya aina hii kama mbingu inavyonga'a kwa nyota mbali mbali. Naweza kusema kwa haki kwamba jinsi Seyidna Ahmad as alivyompenda Mtume saw kakuna mwingine awezaye kujifananisha naye, wala upendo wake kwa Mtume saw haune mfano katika historia yote ya Kiislam. Mtu yoyote hawezi kupinga kauli hii kuwa: makamu ya Seyidna Ahmad as katika kumpenda Mtume saw iko juu zaidi hata kuliko aqili na fahamu ya watu.Wallahi1 mapenzi na Ikhlasi yake kwa mtume saw haina mwisho wake,na

Endelea uk. 10

Hazina ya Mapenzi ni Khilafat Ahmadiyya uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kitabu Chako

Tabia ya kusoma vitabu ni moja ya tunu maridhawa katika maisha ya binadamu. Neno la kwanza kwa Mbora wa viumbe wote, Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. lilikuwa SOMA. Utamu huu unaongezeka mara dufu unaposoma kitabu unachoweza kutangaza kadamnasi HIKI CHANGU nilichonunua kwa jasho langu. Kitabu cha kuazima ni kama mgeni nyumbani, lazima atunzwe kwa heshima na tahadhari. Mgeni wingu la mvua ati!

Tatizo la kitabu cha kuazima huwezi kuranda na kuwanda, huwezi kukiteua unavyotaka, huwezi kuweka alama, ole wako kipasuke au kimwagikiwe maji, utaula wa chuya kwa uvivu wa kuchagua, safari hii sio kuchagua bali kutonunua chako! Usidhani haya ni masimango Rabi Apishe baidi, lakini siku moja ingawaje hilo halifanyiki mara kwa mara unapolazimika kukirudisha kitabu hicho kwa mwenyewe.

Kitabu chako mwenye ahlan wa sahlan unafanya unavyotaka. Vitabu ni kwa ajili ya matumizi, sio kwa ajili ya zinati, kuonyesha. Usiwe na kitabu unachoogopa kuweka alama. Sababu nzuri ya kuweka alama inakukumbusha mahali muhimu katika kitabu na unapata msaada ukitaka kunukuu. Alama inakukumbusha mahali ulipowahi kutembelea zamani.

Ni jambo jema kuanza kukusanya vitabu vipya na vilivyochapishwa zamani. Ya kale ni dhahabu. Jiwekee maktaba ndogo nyumbani, vina mvuto wa ajabu vitabu.

Ulimwengu huu wa leo wa kila mtu na hamsini zake hakuna rafiki mzuri kuliko kitabu. Kamwe hutozozana naye. Na mshairi mmoja aliwahi kusema kitabu kwa siku humfukuza adui ujinga. Kitabu mkononi pia hupunguza porojo zisizo na tija.

Bila shaka mgeni akiona maktaba hiyo atakuuliza "umekwishasoma vitabu vyote hivi?" Nawe uwe na furaha ya kumwambia, "kila kitabu nimekisoma mara tatu".

Ujumbe Maalum toka kwa Hudhur*atba*

Kutoka uk. 1

kusaliwa kwa sura ya watu wakifika kwa kukusanyika. Hivyo, wanajumuiya wanapaswa kusalisha sala ya jamaa majumbani. Wanafamilia wasali Sala ya Ijumaa pia kwa pamoja. Hotuba inaweza kutolewa kwa kusoma nukuu yoyote kutoka katika *Malfuzat* au vitabu vya Jumuiya au vitabu vingine vya Masihi Aliyeahidiwa*as* au gazeti la *AlFazal* au *AlHakam* au jarida lingine lolote na kijana au mwanaume yeyote wa nyumbani anaweza kusalisha Sala ya Ijumaa na pia sala nyingine.

Kwa vyovyote Sala ya Ijumaa haiwezi kutelekezwa kwa muda mrefu. Watu watakaposalisha Sala ya Ijumaa nyumbani na kuandaa hotuba watasoma (vitabu). Hii itaongeza maarifa na hivyo kukaa nyumbani kutokana na maagizo ya Serikali kutasababisha manufaa ya kidini, kiroho na kielimu. Pia, siku hizi gazeti la *AlHakam* limeanzisha safu ya maoni ya watu kwamba sisi tunatumia vipi muda wetu nyumbani kutokana na maagizo hayo; watu wengi wanaandika humo kuwa sisi tunajiongezea maarifa kwa kusoma Qur'an tukufu, Hadithi, vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa*as* na vitabu vingine vya Jumuiya. Watu wengine wa kidunia pia wanatoa maoni yao katika tovuti mbalimbali kuwa kwa sababu hii tumepata nafasi ya kuboresha hali zetu na za familia zetu na maisha yetu ya kifamilia yametiliwa uhai tena.

Sisi pia tunatakiwa kujitahidi kutumia muda wetu huku tukiboresha maisha yetu ya kifamilia na kulea watoto vizuri. Vipindi vizuri sana hurushwa kupitia MTA, tumieni muda walau kidogo kuvitazama kwa kukaa pamoja.

Aidha, kama nilivyokwisha sema, zingatieni barabara maagizo na kanuni zote zilizoundwa na Serikali kwa ajili ya manufaa ya umma na afya yenu; na kama nilivyosema katika hotuba zilizopita kuwa jambo la muhimu kuliko yote ni kufanya maombi kwa makini sana. Tunaweza kuvuta fadhila za Allah*subhanahu wataala* kwa maombi na kuboresha hali yetu ya kiroho na kimwili. Hizi ndizo nasaha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa*as* alizotutolea mara kwa mara; na hata katika hali kama hii alisihi kuwa jambo la muhimu ndilo hili kuwa kuomba msamaha wa madhambi kutoka kwa Allah, kusafisha moyo na kushughulika katika kufanya mema. Allah Ametupatia silaha moja adhimu ya maombi ambayo kwayo tunatakiwa kujitahidi kuwa chini ya himaya ya Allah na kuelekea kwake.

Kuhusiana na kutokusali Sala ya Ijumaa, imeelezwa kwa mujibu wa baadhi ya Hadithi kwamba sala ya jamaa na Sala ya Ijumaa inaweza kutelekezwa kutokana na dharura fulani. Kwa mathalani, Hadithi moja imepokewa katika kitabu cha *Bukhari* kuwa Hadhrat Ibni Abbas*ra* alimwambia mwadhini wake siku ya mvua kwamba "usiseme *'Hayya alasalaat'* baada ya kusema *'Ashhadu an la ilaha ilallahu'* na *'Ashhadu anna Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu'* bali sema maneno haya '***Salluu fi Buyutikum***' yaani **salieni majumbani mwenu**. Msimuliaji akasema: Watu wakaliona ni jambo jipya ndipo Hadhrat Ibni Abbas*ra* akasema: Je, mnashangaa jambo hili? Alilitekeleza aliyekuwa bora kuliko mimi. Ingawa ni muhimu kusali Sala ya Ijumaa lakini sipendi kuwatoeni katika majumba yenu huku mkitembea kwenye mvua na matope."

Allama Imam Nawawi akifafanua Hadithi hii anaandika kwamba hoja ya kuacha Sala ya Ijumaa kutokana na udhuru wa mvua n.k. imo ndani ya Hadithi hii. Hii ndiyo rai yetu na ya wanazuoni wengine ingawa Imam Malik ana rai tofauti na hiyo. Lakini Allah ndiye Anajua lifaalo zaidi.

Vilevile, wanazuoni walijumuisha ugonjwa ambao kutokana nao ni vigumu kuhudhuria msikitini katika sababu za kutokusali Sala ya Ijumaa na sala ya jamaa; na wakadai hoja yake kuwa ni kauli ya Allah*subhanahu wataala* kwamba 'Allah Hakuweka juu yenu udhia wowote katika dini'. Kwa msingi huu Mtume Mtukufu*saw* alipoumwa aliacha kwenda msikitini na akamwambia Hadhrat Abu Bakr*ra* kuongoza sala. Hadithi hii imepokewa katika kitabu cha *Sahih Bukhari* na pia katika kitabu cha *Muslim*. Halikadhalika, mtu anayehofia kuibuka kwa ugonjwa pia anaruhusiwa; na hoja yake ni Hadithi iliyosimuliwa na Hadhrat Ibni Abbas*ra* ambamo Mtume Mtukufu*saw* alieleza **hofu** na **ugonjwa** kuwa udhuru. Hadithi hii inapatikana katika kitabu cha *Sunan Abi Daud*.

Kwa hiyo, ugonjwa huu ambao ipo hatari ya kuenea kwake na Serikali pia imeutolea maagizo maalum ambayo ni muhimu kuyazingatia; katika hali hii ni vigumu kukusanyika mahala pamoja na kusali Sala ya Ijumaa. Lakini kama nilivyosema ***jengeni kawaida ya kusali sala ya jamaa majumbani ili watoto pia waelewe umuhimu wa sala na pia umuhimu wa kusali pamoja na jamaa***. Kutokana na hali halisi ya siku hizi hatuwezi kwenda msikitini lakini ni lazima kutekeleza wajibu wetu huu majumbani kwetu. Zinagtieni sana hilo. Mara kadhaa ilitokea pia katika safari za Hadhrat Masihi aliyeahidiwa*as* ambapo hakusali Sala ya Ijumaa. Aidha, zipo Hadithi nyingi ambazo inabainishwa kuwa si sahihi kukusanyika wakati wa maradhi ya kuambukiza au kukutana wakati wa ugonjwa; na kwa hiyo yapaswa kutengana. Hata hivyo, kama nilivyosema awali hatuitelekezi kabisa bali tunapendekeza njia mbadala ambayo ni kusali majubani. Mimi pia nitajitahidi kufanya mpango kwa ajili yake.

Ombeni kuwa Allah Ashushe fadhila zake, Aufutilie mbali ugonjwa huu duniani, Aifanye dunia itekeleze haki za binadamu na wote wamtambue Allah. Allah Atujaalie sote kutekeleza hilo. Assalamu alaikum warahmatullahi wabarakatuhu."

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Hadhrat Amman Jaan[ra]

Na Sheikh Abid Mahmood Butt
Jalsa Salana Tanzania 2019

Kutoka toleo Lililopita

Subira Na Uvumilivu Wake Wakati Wa Msiba

Bila shaka sote tunafahamu uchungu na wakati mgumu tunaokutana nao katika maisha yetu hususan katika kipindi cha msiba na ule kuondokewa na wapenzi wetu.Huu ni wakati mtu ambao mtu anaweza kutamka yanayomuudhi Mola wake.Lakini hali ni tofauti kwa Hazrat Amma Jaan sahiba[ra] mama huyo alikuwa ni mwenye subira wakati wote wa ugonjwa wa Hazrat Masihil Mau'ud[as] na mpaka katika kifo chake.

Inaelezwa kuwa wakati Masihil Mau'ud[as] alipokuwa anaumwa, mama huyo alifanya maombi kwa unyenyekevu sana na alisema, "Ee Mola wangu uhai wangu umpe yeye". Na alipokuwa mahututi mama huyu akasema, "Ee Allah, bila shaka mja wako huyu anatuacha ila wewe usituache". Na alipofariki, Hazrat Amma Jaan alisema tu "Inna lillahi wa innaa ilaihir raajiuun".

Kina mama walipoanza kulia kwa sauti kubwa, yeye aliwatuliza na kusema, "mimi mwenyewe ambaye ni mkewe sijalia kwa kiasi hicho, inakuwaje nyinyi mlie hivyo".

Kuhusu watoto wake aliwaambia "enyi watoto wangu msidhani baba yenu hakuacha chochote kwa ajili yenu kwa kuona nyumba haina mali mule, amewaachieni hazina kubwa ya maombi ambayo mtaendelea kuyapata maishani mwenu sawa na wakati".

Mwili wa Masihi Aliyeahidiwa ulipowekwa karibu na Bahishti maqbarah, Hazrat Amma Jaan[ra] alisema kwa heshima,"kwa ajili yako malaika walikuwa wanashuka nyumbani mwangu na Allah alikuwa anaongea ".Na baada ya mazishi kila siku asubuhi alikuwa anaenda kaburini pake na kumwombea.

Utii Na Ukaribu Wake Kwa Khalifa Wa Zama

Mwenyezi Mungu anasema;-

Enyi mlioamini! Mtiini Allah na mtiini Mtume wake na wale wenye mamlaka juu yenu. {4:60}

Hadhrat Amma Jaan[ra] alikuwa anauamini uhalifa kwa moyo wake wote na aliona ni faradhi kwake kutii amri na maagizo ya Khalifa wa zama. Hadhrat Khalifatul masih wa kwanza Maulana Hkeem Nuruddin[ra] anasema; "Utii waouomyesha Hadhrat Amma Jaan ma Miani Mahmood[ra] {Khalifa mtukufu wa pili waati kbal hajawea Khalifa} ni wa pekee, na hakuna yeyote aliyepata kunitii nkiasi hicho." Siku moja Hadhrat Khalifatul masihi wa kwanza[ra] alimkabidhi Hadhrat Sufii Ghulam sahib wa Amrat sar mablanketi kadhaa na akamwambia ampelekee Hadhrat Amma Jaam[ra] ili ayashone, Hadhrat Sufii sahib alishtuka na kuhuzunika kuona kuwa Khalifa anampa kazi Ummul-Muminiina ambayo kwa heshima aliyonayo hakustahili kupewa kazi hiyo. Maulana Nuruddin[ra] aliona hali hiyo ya huzuni usoni mwa Hadhrat Sufi sahib lakini alisistiza kwa kusema "mpelekee tu kwani yeye {Amma Jaan[ra]} ameniambia niwe nampa baadhi ya kazi ile afanye, hivyo usiwe na wasiwas." Basi Hadhrat Sufi sahib akazipeleka na baada ya kushonwa akazirudisha.

Katika tukio jimgine imeelezwa kuwa , siku moja Hadhrat Khalifatul masih wa kwanza[ra] alimshauri Hadhrat Amma Jaan[ra] ya kuwa ajenge ukaribu na kina mama wa familia yake {Amma Jaan[ra]} ambao sio waahmadiyya, akamweleza kuwa awatembelee na kisha awaalike waje wamtembelee. Hadhrat Amma Jaan[ra] akatekeleze ushauri huo na matokeo yake ni kwamba kinamama wengi katin yao walijiunga na Jamaat kwa fadhili za Allah.

Inasimuliwa kuwa ilikuwa ni kawaida ya Amma Jaan[ra] kuomba ruhusa kila alipoyaka kutoka nje kutoka nyumbani na hata hivyo alifanya hivyo hata katika zama za Khalifa mtukufu wa pili Hadhrat Mirza Bashruddin Mahmood Ahmad[ra] ambaye ni mtoto wake.

Bila shaka huu ni mfano mzuri na wa aina yake kwa wanawake wa kiahmadiyya na waahmadiyya wote kwa ujumla pindi watoto wewtu wanapobeba dhamana ya uongozi ni wajibu wetu kuwatii na kuwasidia katika majukumu yao.

Kujitolea Kwake Katika Njia Ya Allah

Kwa upande wa kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu,mama huyu hakubaki nyuma hata kidogo.Yeye alijitolea sana tena kwa shauku kubwa kabisa,na mifano michache ifuatayo inathibitisha jambo hili:-

(a) Wakati Hazrat Masihil-Mau'ud[as] alipoanzisha mpango wa kujenga Minaaratul-masih, alimwamuru mtumishi mmoja awatangazie wanajumuiya ya kwamba kila mmoja yampasa achangie rupia mia moja. Akiitikia wito huu,Hazrat Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] aliahidi kutoa rupia elfu moja na alilipa baada ya kuuza eneo lake (ardhi) la urithi huko Delhi.

(b) Mnamo mwaka 1934 wakati Hazrat Khalifatul Masih II Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra] alipoanzisha mpango maalum wa Tahrik-e-Jadeed na kumtaka mwanajumuiya kujitolea, basi Hazrat Amma Jaan[ra] naye alijitolea sana kutoka daftari la kwanza hadi kufariki kwake. Alikua anachangia takriban rupia elfu tatu mia moja arubaini na mbili (3,142). (Seerat Amma Jaan uk.27)

(c) Mfano hai mwingine unaothibitisha kujitolea kwake katika njia ya Allah ni ule unaopatikana katika tukio moja lililojitokeza katika Jalsa Salana ya mwanzo, kama itakumbukwa kwa Jalsa Salana za mwanzo ziliendeshwa na Hazrat Masihi-mau'ud[as] mwenyewe.Siku moja wakati wa Jalsa, Hazrat Mir Nasri Nawaab[ra] aliyekuwa baba wa Hazrat Amma Jaan[ra] alimtaarifu Hazrat Masihil-mau'ud[as] ya kuwa chakula cha jioni kwa ajili ya wageni hakipo. Hazrat Masihil-mau'ud[as] alimwagiza Hazrat Mir Nasri Nawaab sahib[ra] akamwaambie Hazrat Sayyida Nusrat Jahan Begum[ra]. Naye Hazrat Amma Jaan[ra] alimpa baba yake baaadhi ya vitu vyake vya mapambo ya dhahabu, naye akaviuza na pesa hiyo ilitumika kwa ajili ya kuhudumia wageni walioshiriki katika Jalsa Salana hiyo.

Kuwasaidia Wenye Shida

Mwenyezi Mungu Ametuhimiza kuwasaidia ndugu jamaa na wasiojiweza. Katika uwanja huu Hadhrat Amma Jaan[ra] katu hakubaki nyuma, kuna mengi aliyoyafanya kuhusu somo hili, lakini tukio lifuatalo linatuthibitishia kuona kuwa alikuwa mtu wa namna gani.

Hadhrat Maulana Abdur-Rahim Sharma sahib anasema ya kuwa, Hadhrat Mirza Sharif Ahmad[ra] (mtoto wa Hadhrat Amma Jaan[ra]) alinipatia sehemu ya kuishi mimi na familia yangu katika nyumba yake kubwa. Familia yangu ilikuwa na watu watano jumla, mshahara niliokuwa nikipata ulikuwa ni mdogo sana na haukuweza kukidhi mahitaji ya familia, tulikuwa tukitumia nusu (1/2) lita ya maziwa kwa familia nzima.

Habari hii ilivyomfikia Hadhrat Amma Jaan[ra] basi akaamua kutupatia ng'ombe mmoja maalum (yaani ng'ombe mwenye sifa ya kutoa maziwa mengi kama lita saba hadi nane hivi) kwa ajili ya familia yangu. Kuanzia hapo hali katika familia yangu ilibadilika na ikawa nzuri sana.

Jinsi Alivyowajali Watumishi Wake.

Kuwajali na kuwatendea wema watumishi ni agizo la Mtume mtukufu[saw]. Katika hili Hadhrat Amma Jaan[ra] ametuachia mfano mzuri sana. Inasimuliwa kuwa mama mmoja alimwambia Hadhrat Amma Jaan[ra] ya kwamba mtumishi fulani mwanamke (alimtaja kwa jina) anasema chakula anachopata hakimtoshi. Inasemekana kuwa mtumishi huyo alikuwa na mtoto na ndiyo sababu chakula anachopata hakimtoshi, basi Hadhrat Amma Jaan[ra] akamuongezea mchuzi na chapati nyingine mbili zaidi na akamtunzia katika kitambaa chake,na mtumishi huyo alipokuja,hadhrat amma jaan[ra] akamwambia

"chakula chako nimekutunzia katika kitambaa changu,nenda ukachukue." na huko akawaagiza watumishi wengine kwamba yeye ana watoto, msiwe mnampa chakula kidogo kisichomtosha.

Kuwajali Na Kuwahudumia Mayatima

Hazrat Sayyida Nusrat Jahan Begum sahiba[ra] aliwajali sana mayatima na hasa wale mayatima wa kike,aliwalea kwa mapenzi makubwa sana na aliwatendea vizuri sana,aliwalea kama watoto wake wa kuwazaa,aliwaogesha mwenyewe na kuwapaka mafuta na wakati anafanya hivyo uso wake ulikuwa na furaha sana.

Alipoona watoto yatima wameanza kujitambua alianza kuwafundisha kalima tukufu:-Laa ilaaha illa-allahu Muhammadur-rasuulullah,na kisha aliwafundisha sala pamoja na maana yake.Msingi wa elimu ya dini aliwapatia mwenyewe na baadaye alimtafuta mwalimu wa kike ili kuwafundisha Qurani Tukufu mpaka mwisho, pia aliwapeleka shule ili kupata elimu ya dunia na pia aliwafundisha Kiurdu na vitabu vya Hazrat Masihil-mau'ud[as] na kuwaelezea maana yake.

Siku moja Hadhrat Amma Jaan sahibah alikuwa anafanya mazoezi ya kutembea wakati wa asubuhi na pamoja naye walikuwepo kina mama wawili ambao ni watumishi wake. Katika matembezi hayo walifika hadi kijiji cha jirani, huko walimkuta binti wa umri wa kati ya miaka mitano au sita hivi akiwa anakula tunda lililooza katika rundo la taka. Binti huyo alikuwa amevaa nguo chafu sana na ambazo zilikuwa zimechanikachanika. Hadhrat Amma Jaan[ra] akauliza "huyu ni nani?" akawaambiwa huyu ni yatima na pia ana tatizo la kutosikia (kiziwi) na kutoongea (bubu) Hadhrat Amma Jaan[ra] akamwambia mtumishi wake amchukue na wakaja naye Qadian, alipofika akampeleka katika shule ya wasichana iliyokuwa karibu na nyumba ya Hadhrat Masih Mau'ud[as]. walipofika hapo shuleni weanafunzi (waliogopa), Hadhrat Amma Jaan[ra] akawaambia msimwogope huyu ni mwenzenu na nyinyi ndio mnatakiwa mumfanye aonekane kuwa mwanadamu. Akamwambia mwalim amuogeshe na yeye mwenyewe (Hadhrat Amma Jaan[ra]) akaleta kitana na kumchana nywele na kumpaka mafuta na akamvisha nguo nzuri za thamani kubwa, akawa nadhifu na wa kupendeza. Pamoja na kuwa binti huyo alikuwa akihudumiwa na wafanya kazi, lakini kila baada ya siku mbili au tatu Hadhrat Amma Jaan[ra] mwenyewe alikuwa akimwogesha, kumpaka mafuta, kumchana nywele na kumbadilisha nguo. Alipopata makamo alianza kazi ndogondogo. Aliendelea kukua katika hali nadhifu na kupendeza na alipobaleghe, Hadhrat Amma Jaan[ra] akamwoza na kugharamia ndoa hiyo na sherehe zake.

Ukarimu Wake Kwa Wageni

Hazrat Amma Jaan sahiba[ra] alikuwa mkarimu mno kwa wageni,kila aliyekuja alimhudumia ipasavyo na kila mmoja alimhudumia sawa na mahitaji yake.

Hazrat Choudhry Fateh Muhammad Sayyal[ra],alipokuja mara ya kwanza Qadian,wakati huo hasa Hazrat Amma Jaan sahiba[ra] alikuwa akishiriki hasa kuwahudumia wageni.Wageni wote wa kiume walikuwa wakikaa pamoja na Hazrat Masihil-mau'ud[as].Siku ya kwanza bwana Choudhry sahib[ra] akiwa Qadian baada ya kumaliza kula,Hazrat Amma Jaan sahiba[ra] alimtuma mtu kwenda kuuliza kama kuna mgeni yeyote anahitaji chochote basi aseme.Basi hazarat Choudhry Fateh Muhammad Sayyal[ra] akasema yeye amezoea maziwa ya mtindi basi hazrat amman jaan[ra]. akaandaa hiyo na kumpatia na wageni wengine pia kila mmoja alisema alichotaka na akapatiwa.

Inaelezwa kuwa Hadhrat Sayyida Nusrat Jehan Begum sahibah[ra] alipenda kuishi vizuri na mayatima, ndugu na jamaa. Alikuwa na kawaida ya kuwaita ndugu nyumbani kwake na kuwaandalia chakula kizuri walichokipenda na alikuwa akifanya hivyo katika siku kuu za siku za Idi pia. Umri wake ulipozidi kuwa mzee, Hadhrat Amma Jaan[ra] alimwita Hadhrat Bashir Ahmad[ra] na akamwambia, "natamani nimpate mtu nimpe fedha ili aandae tafrija nzuri kwa ajili ya wana familia (ukoo) wote." Naye Hadhrat Mirza Bashir Ahmad[ra] akawa tayari kwa kazi hiyo, basi mama yake (Hadhrat Amma Jaan[ra]) akampa fedha kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo. Somo tunalopata katika tukio hili ni njia bora ya kuimarisha undugu wa familia na ukoo kwa ujumla.

Itaendelea toleo Lijalo

Adamu: Nabii wa Kwanza Duniani, Si wa Kwanza Kuumbwa

Kutoka toleo lililopita

Na **Bw. Juma Iddy Abeid, Kigoma**

Na Adam akawa mtu wa kwanza kuumbwa rasmi kama Nabii kwani baada ya hapo Mwenyezi Mungu Alianza kuleta Manabii kati yao.

Manabii hao walijitambulisha kuwa wametokana na Adam[as] si kwa namna nyingine ila kisa maudhui yao kiroho. Tofauti na wale walio mpinga Adam maana wao baadae walishindwa kujitambulisha kama majini waliopinga wakati wa Adam[as] au mashetani (wapotezaji). Je kwa nini Manabii wao waliweza kujitambulisha? kwa sababu kila Nabii anafunuliwa ili kusaidia kutunza mageuzi ya kiakili na ya kiroho ya Mwanaadamu.

Wale ambao wanapinga hatua ya pili ya mageuzi na wasiokubali kuzingatia mapungufu na kanuni ambazo Mungu ameweka kwa Nabii ili kusaidia mchakato wa mageuzi humkataa Nabii hawatajua hekima yake.

Kwa ufupi waalimu wa Qur'an wanaopinga uwepo wa watu wengine kabla ya Adam wanafikiri kuwa watu wote walikua na akili kama tulizo nazo leo. Pia miili isiyo na manyoya mengi kama tuliyo nay oleo, jambo ambalo ni kutotambua hakika yake.

Laiti wangetambua uumbaji wa kimwili ni matokeo yaliyopita mizunguko ya kimchakato wa mageuzi na kwa maana ya zama ndivyo ili kuwa chanzo cha maendeleo yake ya kiakili pia. Hivyo watu wa kabla ya Adam walikuwa chini sana kufahamu. Walitambulika kama majitu jitu tu, hata akili zao zilikuwa na uwezo mdogo tu.

Inaonyesha kilichowachanganya masheikh wengi ni kushindwa kujua hekima ya Qur'an. Na ndio maana Mwenyezi Mungu anajisifu katika sura 2:27:- *Hakika Allah haoni haya kutoa mfano hata wa mbu na ulio wa zaidi yake. Ama waaminio, basi wanajua ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wao; lakini wale waliokufuru husema: Ni nini Analotaka Allah kwa mfano huu? Huwapoteza wengi kwa huo na Huwaongoza wengi wengi kwa huo; lakini Hapotezi yeyote kwa (mfano) huo isipokuwa wavunjao amri.*

Hakika mifano yote hiyo ilikuwa inalenga zama zinazo tuhusu sisi wakati wa mtume Muhammad[saw], ni mtume Muhammad[saw] ndio ukamilisho wa udhuhirisho wa Adam[as] na watu wakalam wa elimu ya kiduniani wa zama za mtume Muhammad[saw] kuwa dhihirisho la majini zama za Nabii Adam[as].

Ikiwa na maana maneno mengi yanayo muhusu Nabii Adam[as] yalikuwa yatamuhusu mtume Muhammad[saw] ili kumuonyesha hatuna jipya kwake ila yaliyotokea zama za Adam[as]

Isitoshe wataalamu wa leo wamekuwa na majina mengi ya wataaluma tofauti na zama za Adam[as] lakini ukijifunza kupitia wanataaluma hao utapata radha ya Qur'an juu ya majini katika zama za Nabii Adam[as].

Mfano mfupi ni jinni wa masumulizi ambae alitajwa katika Qur'an tukufu kuwa IBLISI alikuwa miongoni mwa majini. Huyu alijiona ni bora na akasema yeye ameumbwa kwa ndimi za moto. Maneno hayo ukiyaangalia ndio marejeo ya leo kwa watu wakubwa wenye umaarufu watu wenye upeo mkubwa.

Tunayajua hayo kutokana na ukweli wa mambo yanayodhihiri sasa. Tazama jinsi kani ya mwendo wa kupaa angani tunavyo hitaji miripuko mikubwa ya moto. Ni miripuko hiyo ndiyo inayo safirisha vyombo angani.

Kwa hali hiyo ni wazi kuwa katika zama za mwanzo watu walishindwa kujua falsafa ya Qur'an kuhusu neno kubwa kwa ndimi za moto kwa JINI. Kiupana 'KWA NDIMI ZA MOTO' kueleweka kwa upana na liendane na uvumbuzi wa kisayansi ya Mwanaadam na ndio itakuwa heshima kuwa kuwa Qur'an tukufu. Na heshima kwa Mtume Muhammad[saw].

Je! Ni heshima gani hiyo. Ni wazi wenye upeo walio mkatalia Nabii Adam watakuwa tofauti na wakati wa Mtume Muhammad[saw], Qur'an inasema kundi moja la majini walisikia Qur'an wakaamini. Maana yake zama za wataalam wataikubali Qur'an katika nyanjan mbalimbali kuwa ni kitabu sahihi.

Na hiyo ni tofauti na hadithi yamajini ya *Alif lela ulela* iliyotungwa Baghdad ya viumbe vya kufikirika. Mfano tujalie kuwepo viumbe hao na wasalimu au kama Mwenyezi Mungu Alivyosema "*Sikuwaumba majini na watu ila wapate Kuniabudu*."

Ikiwa wako tofauti na sisi kuna mtu kazaa lazima yaoate majibu ya kina. Maana inasemwa majini yaliumbwa kabla ya watu, hivyo ni lazima:-

- Yawe na umbile la kinamna Fulani
- Yafikishiwe mwongozo
- Lazima yawe chini ya sheria
- Yawajibike katika utoaji wa zaka na sadaka
- Watapaswa kuwajibishwa katika hukumu na tabia za uzinzi, wizi n.k

Je! Nani atakuwa DAI ILA LAH kwao na jinsi gani ujumbe utafikishwa kwao. Wanahusishwa vipi katika ndoa na mirathi kwa misingi ya Islamu. Hayo ni ya msingi kabla ya kukubali hadithi zao za kufisadikishwa maana sura 6:131 :- *Enyi makundi ya majinni na wanAdamu! Je hawakuwafikieni Mitume toka miongoni mwenu kuwabainishieni Aya Zangu na kuwaonyeni juu ya mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.*

Ni wazi aya inaonyesha makundi yote mawili walifikiwa na mwongozo ila ajabu Manabii wanapatikana katika kundi la watu. Na Waislam tunafahamu kwa majina toka kwanza Adam[as] hadi wa mwisho kwa kuongoza Muhammad[saw]., Je! Orodha ya makundi ya majini ilikuwa na orodha ya Manabii wangapi. Hilo ndilo la kutafakari.

Majina Ibilisi, Mwanadamu na Majini Yanatokana na Hekima ya Qur'an katika Zama Zetu

Kwa kuwa Ibilisi alikuwa mmoja wa jinni ndio kusema ni sifa iliyo muhusu muhusika mmoja. Abu jahili alikuwa mpingaji mkubwa zama za mtume Muhammad[saw] huyo alitambuliwa kama mtu mwenye elimu kubwa na hekima mno, yeye aliyefananishwa ndani ya Qur'an kama mwakilishi wa mtu aliyeitwa Ibilisi zama za Nabii Adam[as]

Ibilisi hapo awali haikuwa sifa ila jina la asili la mtu na ndio maana hatumkuti akitajwa tena ya Qur'an pasipo zama za Adam[as] na jinni iliwakilisha uwezo wake wa utambuzi wa kuwa na akili ya hali ya juu, hivyo Mwenyezi Mungu Alikusudia kumfahamisha kuwa kupingwa kwake hakuna tofauti na zama za Nabii Adam. Tofauti ni kuwa toka mwanzo Mwenyezi Mungu Aliahidi kuwa katika wafuasi wa Adamu nao wataendeleza silisila ya kusadikisha uwepo wa Mwenyezi Mungu wa kuwaongoza wanaAdam 7:36 :- *Enyi wanAdamu, bila shaka watawafikieni Mitume kutoka miongoni mwenu, watawaelezeni Aya Zangu. Basi atakayeogopa na kufanya wema, haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.*

Ahadi hii ni ahadi endelevu, maana majini na watu katika zama zijazo zitakuwa zama zenye upana wa maendeleo. Kwani kwa zama za kale ingekuwa ngumu kuelekea Zaidi ya kubuni visa vya ajabu juu ya ajabu.

Mfano 55:34 :- *Enyi jamii ya majinni na watu, kama mkiweza kupita kando za mbingu na ardhi, basi piteni; lakini hamtapita ila kwa idhini.*

Je! Zama hizo kulikuwa kuna nyenzo gani za watu na majini kuweza kwenda mbinguni.?

72:2:- *Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi la majinni walisikia wakasema: Hakika Tumesikia Qur'an ya ajabu,*

Bila shaka hizo zilikuwa zama mpya za Nabii wa kwanza kuumbwa kwa kupewa sheriya na zama za Nabii wa mwisho kupewa sheriya. Si zama za mtu wa kwanza kuumbwa na mtu wa mwisho kuumbwa.

Ndio maana majini ya zama za Adam wao waligoma kumtii Nabii wao. IBILISI alipogoma akawa miongoni mwa wadhalimu hao. Majigambo ilikuwa ni kuumbwa kwa ndimi za moto na kutomtii aliyeumbwa kwa udongo. Ukitazama juu juu huwezi kupata radha ya kurani tukufu nautabaki na mawazo ya elif lela za hekaya za Abunuasi.

Mfano 72:7 -: *Na hakika kulikuwa na watu miongoni mwa wanAdamu wakijikinga kwa watu miongoni mwa majinni, hivyo wakawazidishia kiburi.*

Ukiona aya hiyo utaona viumbe vitatu jambo ambalo itakuwa ni vichekesho. JINI, MWANADAMU NA MTU ilihali ni sifa tu ya kiumbe mmoja.

Ila migawanyo ya vipawa vimesababisha sifa kuwa tofauti na kulingana na zama pia Qur'an iliashiria zama ambazo ulimwengu utakapogawanywa makundi matatu. Kama tulivyo leo tayari sote tumekubaliana kuwa kuna ulimwengu wa kwanza, ulimwengu wa pili na ulimwengu wa tatu. Katika makundi hayo matatu, kundi la ulimwengu wa kwanza ni kundi la watu wenye nguvu ya kutumia moto, ambao wamekuwa maarufu na nguvu zao zimefichikana watu kuziona na kuiga. Watu hao wanaishi ulimwengu wa majini kwa kuwa na sifa ya ulimwengu wa kwanza.

Halafu wapo watu wa kawaida ambao wao wanaishi kwa maumbile yenye kubadilishwa kadri yatakavyopangwa na wengine, hao wapo ulimwengu wa tatu ambao wana sifa ya udongo wa ufinyanzi.

Ni wazi katika zama za mwanzo watu walishindwa kujua falsafa ya Qur'an ya neno jini au ndimi za moto kwa namna ya upana lakini sasa ni lazima neno hili JINI kueleweka kwa upana na ili lieleweke ni pale litakapohusishwa na uvumbuzi wa kisayansi ya mwandam na hapo ndio itakuwa heshima kubwa ya Qur'an tukufu.

Zipo aya nyingi ndani ya Qur'an tukufu juu ya majini ila sio makusudio yangu, ila nilicho taka kuwaonyesha tu wasomaji kuwa hakuna tofauti ya IBILISI na ABU JAHAL. Kuwa walikuwa watu wa kawaida na neno jini halikuwa viumbe tofauti kimaumbile ila uwezo wa akili.

Ni kwamba akili ni nguvu isiyoonekana kwa macho nayo pia inatoa matawi mengi ya elimu:- Na akili ndio tunu ya Mwanaadam tofauti na viumbe wengine akili ambayo ukuwaji wake ni wataratibu japo utokea miongoni mwetu tukawashangaa wenzetu waliojaaliwa akili za hali ya juu na kwa muda mchache kiumri, watu ambaowazungu huwaita jimasi.

Kama nilivyo sema awali kuwa Nabii Adam ndiye Nabii ambaye Mwenyezi Mungu alimuumba miongoni mwa zama watu wameanza kupevuka. Wametoka zama za kula matunda na mizizi tu kama nyani wa porini.

Zama za moto zilipo anza wao waliamini wazi ndio wanaostaili kuongoza uma sio mtu kama Adam. Hao wakawa tofauti na majini zama za mtume Muhammad[saw] yaani wao hawatopinga ila watakua wakitakii Qur'an na mafundisho yake kisha watakuwa wakistaajabu jinsi Qur'an inavyo kwenda na zama zao za kiugunduzi mfano leo wameweza kupita juu ya sayari, sayari zilizo kando ya dunia yetu hii kirahisi mwendo wa chombo chap ni moto juu ya moto, mripuko mkubwa kila hatua wanaokwenda. Ndio kusema kila hatua ya Mwanaadam ina mwanzo halisi si mtu halisi.

Itaendelea toleo Lijalo

Hazina ya Mapenzi ni Ukhalifa wa Kiahmadiyya

Na Rajabu Abasi Mkieti
Masjid Salaam, DSM

Kwa fadhila za Allah mnamo 15/02/2020 Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilifanikiwa kuandaa jukwaa la siku moja la kitaifa kwa Maqaid wa mikoa (*1st National Qaideen Forum 2020*)

Katika jukwaa hilo kulifanyika matukio mbalimbali katika kuwajenga na kuwapa viongozi uwezo utakaoendana na mapinduzi makubwa ili kuendana na maendeleo ya dunia ya leo, huku tukibaki katika kumuabudu Allah.

Kauli mbiu ya jukwaa hili ilikuwa ni ***Khilafat Ahmadiyya***. Kauli mbiu hii ilikuwa ni moja ya mada iliyojadiliwa kwa upana zaidi. Mtu ambaye alipewa kazi ya kuhakikisha anawasilisha mada hii alikuwa ni Maulana Sheikh Abdulrahman Ame sahib. Sheikh Ame sahib alifafanua juu ya kiini cha Khilafat Ahmadiyya na majukumu ya kila Muahmadiyya ni kuupenda na kutii na kuufata kinagaubaga katika kila siku za maisha yetu tukiwa kama viongozi wa tanzimu ya Khuddam.

Sheikh Ame alisema *'Makhalifa wa zama ni viongozi wetu wa kiroho, wanaotupatia uongozi wetu wa kila siku lakini kwa hakika wao ni zaidi ya baba zetu waliotuzaa na kama tutafikiria wanaotufanyia hata baba zetu waliotuzaa hawajatufanyia au hawawezi kutufanyia hayo'*. Sheikh sahib alisema hali hii ya kutupenda tunayopata kutoka kwa Makhalifa wa Kiahmadiyya katu haiwezi kufikiwa kutoka kwa wazazi wetu wakipenda au wakitaka hawataweza katu.

Sheikh Ame alieleza njia pekee itakayotufanya tupate maendelo ya kimwili na kiroho ni kuwa karibu na nidhamu hii ya ukhalifa katika zama za dunia ya leo. Alieleza baadhi ya matukio yake binafsi lakini pia ya Jamaati kwa ujumla yanayotuunganisha na Khilafat aliyoyaona kutoka kwa Makhalifa wetu. Tukio moja ambalo alilieleza ni kuwa wa siku moja wakila katika dhifa fulani huko London pamoja na Khalifatul Masih wa nne, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad[ra], mara katika hali isiyo ya kawaida Huzur[rh] akawataka wajumbe wote awapatie *Ice cream* aliyokuwa ametengewa yeye. Hali hii ilimfanya kuona jinsi gani Khalifa pamoja na hali yake anavyojali watu pia alieleza baadhi ya matukio ya kukubaliwa kwa maobi ya Makhalifa na aliwahamasisha viongozi kuhakikisha wanamuandikia barua Khalifatul Masih[atba] na kuangalia MTA na kuona wanawahamasisha wanachama wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya. Sheikh sahib alieleza njia mbalimbali zitakazotufanya kuwa karibu na Ukhalifa tukiwa kama viongozi na kwa hali hiyo tutapata baraka na mapenzi yasiyyo na kikomo kutoka kwa Khalifa wa zama.

Mada nyingine ambazo zilizo jadiliwa zilikua ***Umuhimu wa Kutekeleza Shughuli za Kila Siku Pamoja na Maazimio ya Shura***. ***Nidhamu ya Utoaji Michango Sawa na Kipato katika Miongozo ya Jamaat*** ni moja ya jambo lililopewa kipaumbele zaidi katika jukwaa hilo la siku moja. Idara ya *Waqf-e-Nau* nayo ilipewa nafasi kueleza mikakakti yao katika siku zijazo, kwa hali hiyo katibu wa *Waqf-e-Nau* taifa ndugu Amir Kaluta sahib alieleza kwa mapama juu ya matamanio ya Khalifa wa zama katika idara hii na alisema Khalifatul Masih[atba] anawaomba wanajamati kuwatoa zaidi watoto wao katika mpango huu. Katika kikao hicho katibu wa *Waqf-e-Nau* taifa alitangaza rasmi kuwa Maqaid wa mikoa Majlis Khuddamul Ahmadiyya watakuwa moja kwa moja ni makatibu wa *Waqf-e-Nau* katika mikoa yao.

Swala la nidhamu ya uongozi nalo halikua nyumba kwani katika uongozi ni silaha isiyoisha makali na itakayoleta mapinduzi katika kila hali, kusema kweli na kuishi katika hali hiyo ndio roho ya uongozi.

Ilipofika saa kumi na moja kamili jioni mgeni rasmi ambaye ni Amir na Mbashiri Mkuu, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudry



Wahudhuriaji wa Jukwaa la Qaideen wakifuatilia kwa umakini



Mafunzo kwa wahudhuriaji wa Jukwaa la Qaideen yakitolewa na hadhara kuuliza maswali

waliohudhuria semina hiyo ni viongozi basi kazi hiyo ya kuhakikisha viongozi wanafundwa aliveshwa katibu wa Tabligh taifa ambaye ni Sadr Ansarullah, ndugu Ally Hamisi Mbambwa sahib. Katibu alisema uongozi sio kazi ya mchezo ni jambo linalohitaji msaada wa Allah, kila kiongozi ahakikishe anaomba msaada kutoka kwa Allah. Alisema jambo la changamoto la uongozi ni kawaida, jambo moja kubwa kwa kiongozi ni kuhakikisha unakuwa na msimamo. Taarifa sahib aliingia jukwaani na kukaribishwa na Sadr Khuddamul Ahmadiyya ndugu Ramadhani Nauja sahib. Kikao kiliendelea kwa Sadr Khudam kutoa taarifa fupi ya matukio yaliotekelezwa kwa siku nzima. Sadr Khuddam alisema mikoa iliyoshiriki ni 13 na mikoa ambayo haikushiriki ni 5 kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo. Wajumbe jumla walioshiriki ni 63 na kwa mkoa wa Dar es salaam waliohudhuria ni wajumbe kutoka matawi yote. Pia katika jukwaa hilo lilifanyika tukio la kuwaaga Khuddam 2 waliofikia miaka 40 na kuhamia Majlis Ansarullah ambao walikua ni viongozi wa muda mrefu katika Majlis Khuddam na kupatiwa vyeti vya shukurani kwa majina ni ndugu Yousuph Mgeleka na ndugu Fadhili Ally Namkumbe. Vyeti hivyo vilitolewa na mgeni rasmi.

Amir sahib ambaye alikuwa mgeni rasmi alianza hotuba yake kwa kusoma aya mbalimbali kutoka katika Quran tukufu zinazotukumbusha kujitolea katika njia ya Allah na kuongeza uchamungu. Amir sahib aliongeza kuwa kila kiongozi ahakikishe kuwa njia ya kuhakikisha anafanikiwa ni kusema na kutenda na mwisho aliwaeleza viongozi kuwa tunatakiwa kuhakikisha tunakuwa Waislamu wa matendo na sio wa maneno kwani hii ndio sababu ya kuletwa Masih Aliyeahidiwa[as]. Mwisho Amir sahib alifunga semina hiyo ya kwa maombi.

Upendo na Utii wa Masahaba kwa Mtume[saw]

Kutoka toleo Lililopita

Qurani Tukufu yabainisha jinsi Masahaba walivyoihami dini ya Islam pale iliposema:

"*Na Wafanyieni maandalizi mwezavyo kwa kukusanya nguvu na kwa kufunga farasi mipakani, ambazo kwazo mnawatisha maadui wa Allah na maadui zenu...*" (Al-Anfal: 61) ; na

"Enyi mliomaini, subirini na subirisheni, na kuweni imara katika kuihami mipaka, na mcheni Allah ili mpate kufaulu." (Aal-e-'Imran: 201).

Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema kwamba: Nini mana ya Ribaat? Farasi ambao wamefungwa mipakani mwa adui ndio huitwa Ribaat. Allah Mwenye Enzi Anawaamuru waaminio kujiandaa kumkabili adui wakati wowote. Kwa kupitia neno hili Ribaat, alizielekeza nadhari zao kujiandaa kwa ukweli kabisa. Walipewa majukumu mawili.

Kwanza ni kwa kumkabili adui kinguvu na ya pili kumkabili adui kiroho. Kwa ajili ya mapambano ya kiroho kuna agizo pia la Ribaat, kwamba mtu muda wote awe amejiandaa. Katika kamusi Ribaat pia humaanisha roho na moyo wa mwanadamu, na kwa uhakika hasa ni wale farasi waliofugwa vizuri na waliofunzwa tu ambao wanaweza kufanya hayo.

Siku hizi kufundishwa na kufunzwa kwa farasi kunafanywa kwa njia hii na wao kufugwa na kufundishwa kama watoto wanavyofundishwa kwa hadhari maalum na umakini. Kama wao hawafundishwi, basi hawawezi kufugika na wanakuwa hawana maana kabisa. Badala ya kuwa wenye manufaa wataishia kuogopwa na kuleta madhara.

Kwa hiyo, roho nayo lazima ielekezwe kwa namna hii na kuwekwa chini ya uangalizi na haja ya kuifundisha pia iwepo. Hivyo, Ribaat hutokea tu wakati muumini anapojitahidi kupiga hatua za maendeleo katika utambuzi na matendo mema na kwa kuzidhibiti tamaa zake.

Mwisho

Bustani ya Washairi

NIPE KADIRI YANGU

Eh Mola nipe hima, Na hekima ya maneno
Kazi yetu kuungama, Huwa kama msumeno
Pindi huleta heshima, Wakati twala maneno
Kunipa heshima yangu, Hakukushushi cheo

Kunipa heshima yangu, Huenda kwako mtihani
Ujuzi pia ni fungu, Usitweke kitanzini
Mezidi kipato changu, usinione wa chini
Kunipa heshima yangu, Hakukushushi cheo

Kiongozi Kiongozi, Maamuma maamuma
Ziheshimu hizi ngazi, hubadilika kwa zama
Twapeana kwa vizazi, Sio maji yalotwama
Kunipa heshima yangu, Hakukushushi cheo

Kuchukuliana poa, Kuishi kwa mazoea
Hujali la kuniambia, Ropo waniropokea
Sauti wanipazia, Kweupe bila pazia
Kunipa heshima yangu, Hakukushushi cheo

Ni njia barikiwa, Kutendeana kwa hadhi
Mzee mpe kahawa, na mtoto hawi kadhi
Mwisho wa yangu ngalawa, Jalia Mola Hafidhi
Kunipa heshima yangu, Hakukushushi cheo

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721, shunda267@gmail.com

WENZETU WAMETUTOKA

Nimeishika kalamu, niyaandike ya moyoni
Yametufika magumu, kwa fadhila za Manani
Aliyeumba kaumu, Kaeneza duniani
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Ilikuwa Lihamisi, siku hiyo nabaini
Tarehe ni thelathini, lipoanzia huzuni
Mwezi ni naubaini, ni wa kwanza kwa nambari
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Mzee wetu makini, Bashiri mwana wa Heri
Bila hata ya kuhisi, yalimbana ni maradhi
Ni sitoroko kwa kasi, hiyo ilimkabili
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Ilimfika kwa kasi, ikamtoa uhai
Akatoka duniani, kwa mapenzi ya Jalali
Tulimpenda jamani, Mola Kapenda zaidi
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Kwa fadhila za Kudusi, Uwezo Alitujali
Kufanya Yake Jalali, kumzika kulihali
Ijumaa ya nafasi, tuliifanya faradhi
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Wa pili ninambaini, mmujue kulihali
Huyu naye si mwingine, ni Rashidi wa Kausimba
Tarehe kumi na nane, tukafikwa na msiba
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Kwikwi ilimfikia, ilifika kwa ukali
Walikosa yake dawa, kuuzuia ukali
Mapenzi ya wake Mola, katoa wake uhai
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Kwa fadhila za Manani, mambo mane ya Jalali
Tuliyafanya jamani, kwa njia ya uhalali
Kila mtu abaini, yaliyomo vitabuni
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Tarehe kumi na tisa, mazishi yalifanyika
Kwa dua za kimoyoni, za Manani Mtukuka
Za kumwombea mpendwa, mpendwa wetu Kansimba
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Hali hii ndugu zangu, ni mipango ya Jalali
Tumpende sana Mungu, tupate njema amali
Tuyaepuke magumu, kwa kutumia akili
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Nasi pia tuyajue, sisi pia wa manani
Hili ndugu tulijue, nasi pia tu njiani
Dunia hii tujue, siyo yetu abadani
Wenzetu wametutoka, Mansaru wetu wawili

Hapa kwangu kituoni, tumpende wetu Mola
Tushiriki kwa makini, tuhesabiwe na Ala
Tuwaombee jamani, wapate kufarijika
Kifo kimetangulia, na uhai waja nyuma

Harun R. Bundala
S.L.P. 54, Kiloleni, Tabora

NASUSA

Mola wetu U Ghanii, Mkwasi so mhitaji
Metupa nafasi hii, Tuwe wako waitaji
Ni hisani yako Ngai, Mwisho watuvika taji
Kazi yako sisusii, Mola wetu U Ghanii

Nasusa! Hasara kwangu, Mipango yako yasonga
Nafasi, wapo wenzangu, Kwangu yabaki majanga
Nabaki piga majungu, Kutia watu michanga
Kazi yako sisusii, Mola wetu U Ghanii

Ulisha niweka mbele, ghururi ikanijaa
Rai kaona kelele, Mjuzi wa kila njia
Leo nimiguu chale, Na sina pa kuanzia
Kazi yako sisusii, Mola wetu U Ghanii

Shunda nashundia Wana, Kwa ushairi na tenzi
Mpole na muamana,Mlezi wenye mapenzi
Uongozi ni amana, mgawaji wenye Enzi
Kazi yako sisusii, Mola wetu U Ghanii

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721, shunda267@gmail.com

CORONA

1. Tunakuomba Rabana, tunakesha na kulia
Hatuwezi kulingana, hali ya kuvumilia
Wengi wanalia sana, Kwako wanakimbilia
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

2. Tunusuru Mungu wetu, Corona gonjwa hatari
Sisi hapa ombi letu, tuwe wazima na ari
Samehe kiburi chetu, tunajifanya ngangari
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

3. Hii homa ya mapafu, inaua si kitoto
Tusijiweke upofu, eti haipendi joto
Inaua maelufu, wazee hadi watoto
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

4. Wanakufa watu wengi, wa bara na baharini
Hata wenye pesa mingi, wamekwenda aridhini
Dua ndo wetu msingi, tuwe nje ama ndani
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

5. Ulianzia Uchina, ukaenda Marekani
Ukasambaa kwa sana, ukafika Arabuni
Yarabi toba rabana, Tuokoe duniani
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

6. Ugonjwa huu hatari, unasambaa kwa hewa
Ukijifanya jabari, jiandae kupepewa
Kiumbe acha kiburi, ukipona ni ngekewa
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

7. Ewe ndugu muungwana, kumbuka nawa mikono
Hutakiwi kugusana, wala kushika kiuno
Kupiga chafya hapana, endeleza mapambano
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

8. Kupiga chafya hapana, mana yake ujikinge
Iwe usiku mchana, usije kusema ninge
Mungu Corona hapana, Tuepushe na kilinge
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

9. Embu nawa na sabuni, mikononi kila mara
Usije dhani utani, sikia acha papara
Usijishike usoni, jifute na kitambara
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

10. Na msikumbatiane, kabisa nduguzanguni
Sote tuseme kamwene, tujikinge majumbani
Kisa kuwa na mapene, usiulize kwa nini
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

11. Usiulize kwa nini, mbona ugonjwa hupati
Embu tema mate chini, usijepigwa na shoti
Tukeshe misikitini, tukingojea tamati
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

12. Kukohoa kila mara, mwili kushikwa na homa
Embu wahi maabara, usije kufa mazima
Ni Corona si Ebola, usije fikiri ngoma
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

13. Ukihisi hali hizo, hima jitenge mapema
Na tuweke angalizo, kwa watoto kina mama
Maana dalili ndo hizo, tayari nimeshasema
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

14. Jifunike kitambaa, unapopiga chafiya
Vidudu vikisambaa, utaonekana boya
Embu acha kushangaa, Corona ni gonjwa baya
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

15. Mungu wetu twakuomba, Tuepushe na zahama
Ni lazima kujikomba, na Wewe ndo wetu Bwana
Gonjwa linatufilimba, kupiga kazi hakuna
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

16. Kila homa si Corona, tulia acha papara
Jihadhari embu ona, usije kugaragara
Omba Mungu utapona, usifunge biashara
Corona gonjwa hatari, Tunusuru Mungu wetu.

17. Nimefikia tamati, virago ninafungasha
Nimekumbusha umati, nimesema vya kutosha
Yabidi tujidhatiti, mikono yetu kuosha
Tunakuomba Rabana, Utupatie nusura.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
#MMAKONDE MSOMI
Kalindimasenior@gmail.com

DADA MAYASA

Shemeji yangu mudhamu , Muniri nimepokea
Salamu zilo muhimu, kwa Mnungu familia
Kwa baraka za karimu,Dada amejifungua
Hongera dada mayasa, Mwana umejizalia

Chana chetu kilobora, Mola ilahi tukuzie
Malezi yalo imara, wote sisi tumkidhie
Na mafunzo ya sitara, Ya dini tumpatie
Hongera dada mayasa, Mwana umejizalia

Rabi Mola Jalali, Mudhakiri Mbarikie
Baraka za kila hali, Dini aje aitumikie
Na dunia bilkuli, katu asikumbatie
Hongera dada mayasa, Mwana umejizali

Mwisho hizi salamu, kitonga ziwafikie
Na dutumi mahashumu, nanyi pia mzipokee
Siku moja ikitumu, ataletwa mfurahie
Hongera dada mayasa, Mwana umejizali

Rajabu Abasi Mkieti
AL-WATTANI -_MLEZI
Lusanga Muheza -Tanga

DHIKI

Nitegemeapo Faraja, Dhiki zikinitokea
Ndipo nionapo waja, wote wakinikimbia
Ila Ilahi wa haja, Mola Ananikidhia
Jalilu Mola Karima, yeye ndo namtegemea

Kila siku enyi jama, mimi namuhimidia
Anilinde na zahama, pale inaponizigia
Halipo lakuni kwama, Rabi tanisitiria
Jalilu Mola Karima, yeye ndo namtegemea

Mama yangu bi Rehema, pia Dua namuombea
Maisha yende Salama, ya aghera na dunia
Lisimpate la kumkwama, na nyingi pia fedhea
Jalilu Mola Karima, yeye ndo namtegemea

Rajabu Abasi Mkieti
AL-WATTANI -_MLEZI
Lusanga Muheza –Tanga

Hadithi ya Seremala

Seremala mmoja alikuwa tayari kustaafu, na akamwambia mkuu wake juu ya mipango yake ya kuondoka na kwenda kuishi maisha ya raha pamoja na mke wake. Angeukosa mshahara wake wa mwezi huo, angeweza kusubiria, lakini alihitaji kustaafu.

Mhandisi alisikitika kuona mfanyakazi mzuri namna yake akiondoka, basi akamuomba seremala kutengeneza nyumba moja tu zaidi kama ombi lake binafsi.

Seremala akasema sawa, lakini kadri ya muda ilikuwa rahisi kuona kwamba moyo wake haukuwa katika kazi ile. Akafanya kazi ya stadi mbovu na alitumia malighafi dhaifu. Ilikuwa ni namna mbaya kumaliza kazi yake ya muda mrefu vile.

Seremala alipomaliza kazi yake, mhandisi akaja kuikagua nyumba. Akakabidhi funguo ya mlango wa mbele kwa seremala. "Hii ni nyumba yako," mhandisi alisema. "Ni zawadi yangu kwako."

Seremala alishtushwa! Aibu gani hii? Kama tu angejua alikuwa anatengeneza nyumba yake mwenyewe, angeitengeneza kiupekee kabisa.



Vivyo hivyo na kwetu pia. Tunajenga maisha yetu, kila siku, aghalabu tukiweka juhudi kidogo kuliko uwezo wetu katika mjengo. Kisha kwa mshtuko tunagundua tunabidi tuishi kwenye nyumba tuliyojenga.

Kama tungeweza kujenga tena, tungefanya kwa ufanisi sana. Lakini hatuwezi kurudi nyuma...

Wewe ni seremala wa maisha yako. Kila siku unagongelea msumari, unaweka ubao, au kusimamisha ukuta. Tabia zako na machaguo unayofanya leo hujenga "nyumba" yako ya kesho...

TAFUTA MANENO

QURAN	TAQWA	SIHR	MWAMINIO
SAUMU	HIJA	MAOMBI	MASIHI
TARAWEH	SHAWWAL	DHAMBI	ALFAZL
RAMADAN	DAKU	WEMA	MUSLIH
IKHLAS	FUTURU	FASIKI	MAUUD

Yatafute maneno hapo juu kwa kuyazungushia na Penseli na tambua maana zake.

F	F	U	T	U	R	U	N	B	L	D	B	Q	L	Q
T	T	W	E	M	A	M	N	Z	U	T	Z	X	P	D
T	V	A	Q	F	K	M	A	K	H	W	H	K	N	G
F	F	T	R	N	W	F	A	U	X	N	M	I	R	T
S	L	K	L	A	L	D	N	M	U	D	K	H	J	I
H	Y	B	N	A	W	P	Z	T	M	D	T	M	B	A
A	S	A	U	M	U	E	T	A	Q	W	A	M	T	B
W	M	I	F	M	K	L	H	V	B	Q	A	P	R	N
W	A	X	H	Y	R	F	H	S	H	H	V	T	A	L
A	O	M	Y	R	T	L	A	I	D	X	Q	R	M	Z
L	M	A	B	D	X	L	L	S	L	J	U	R	A	B
V	B	S	W	K	H	S	V	Q	I	Q	Y	W	D	D
C	I	I	N	K	U	B	H	X	R	K	J	Y	H	Q
Q	K	H	I	M	K	H	G	X	J	T	I	C	A	M
J	L	I	X	N	M	W	A	M	I	N	I	O	N	H

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Kupika Keki kwenye Mkaa

Na **Mubarakati S. Mbaruk Kapilima**

As Salaam Alaikum warahmatullahi wabarakatu, leo tutaelekezana jinsi ya kuandaa keki kwenye jiko la mkaa

MAHITAJI

1. Ngano ¼
2. Sukari ¼
3. Blueband 125gm
4. Mayai 4 mpaka 6 kulingana na ukubwa
5. Ladha (Iriki / Vanilla / Fanta Orange) utakayopenda
6. Maziwa ½ kikombe
7. Cocoa kijiko 1½ (ukipenda)
8. Baking powder kijiko 1

MAANDALIZI

1. Washa jiko lako kabisa ili lishike moto mapema
2. Chukua chombo weka blueband na Sukari kisha changanya mpaka vichanganyike
3. Kisha weka yai mojamoja endelea kuchanganya
4. Weka maziwa
5. Weka unga na Ladha uipendayo sababu ya harufu (vanilla / Iriki au yoyote)
6. Gawa vijiko sita pembeni weka cocoa
7. Chukua chombo chako cha kuokea weka mchanganyiko wako mweupe bakisha kidogo
8. Weka mchanganyiko wenye cocoa, malizia na ule mweupe uliobaki
9. Punguza moto jikoni weka juu ya mfuniko bakisha kidogo
10. Tanguliza chombo kikubwa jikoni kisha weka sufuria yako ya keki ndani yake funika kwa muda wa dakika 45

- Ikiwa tayari ipua



Nb: unaweza kutumia kijiti kutazama kama keki yako imeiva

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Je Kila Janga la Asili ni Adhabu?

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

Na Tunapokusudia kuuangamiza mji tunawaachia wenye uwezo wa kiuchumi miongoni mwao kufanya watakavyo. Ndipo wanajiingiza katika mambo yote ya dhambi yaliyo humo, kiasi kwamba sasa inakuwa ni jambo la haki mji huo kuhukumiwa. Kisha Tunauangamiza maangamizo makubwa. (Surat Al-Isra' 17:17)

ADHABU ni Mateso, vifo na Kuharibu Mali kwenye kiwango ambacho uwezo wa binadamu hauna uthibiti nao. Kila kitu ni Rehema ya Allah 7:157 na Adhabu hujulikana baada ya Neema kugeuka kuwa Adhabu. Pale ambapo jambo huhesabika kama maangamio. Kuna maangamio ya mtu mmoja mmoja, kundi, Jamii, Taifa na Dunia yote. Zifuatazo ni baadhi ya sababu ambazo hupelekea maangamio.

1. Mvua kubwa kiasi cha kumeza makazi na vitu vyake (54:10-13)
2. Upepo mkali kiasi cha kuoa uoto wa asili na makazi (54:19-21)
3. Maporomoko ya Mawe ambayo huonekana kama volkano na kuharibi ardhi na makazi yake (15:74-75)
4. Tofani ya Mchanga yenye kurundikana juu ya makazi na kuangamiza kila kilichopo juu ya ardhi (46:25-26)
5. Mafuriko ambayo huondoa Rutuba ambayo hugeuza ardhi tupu isiyo mea chochote cha faida (34:17)
6. Tetemeko la ardhi ambalo huzika makazi na viumbe vingine (91:15)
7. Ukame unaopoteza Maji na udongo kuondokewa na maji kabisa (67:31)
8. Bala la Njaa ambalo hulikabili taifa kwa hofu vifo na taabu (16:113)
9. Vita ambazo huangamiza Taifa na kuongeza ugumu wa maisha, mashaka na Mateso (7:95)
10. Uwepo wa makundi na makundi ya ndege waharibifu ambao hushambulia mimea na vyakula (105:4-6)
11. Kupasuka kwa Mito/ Mabwawa na kuvamia makazi na mashamba (89:14-15)
12. Kuenea kwa Wadudu, mabadiliko ya tabia nchi, ongezeko la Ukame au Unyevunyevu ambao hupelekea kuhatarisha maisha na kuzalisha wadudu wengine wapya wanaosababisha Magonjwa ambayo hayakuwepo na Magonjwa ya Miripuko na husababisha magonjwa ya Damu na kuharibu mfumo wa mzunguko wa damu (7:134)
13. Adhabu inayotokana sio na Imani ila mateso ya watu wako au wengine kwa kuwadhulumu. Hasara na adhabu mbalimbali humkumba ikiwa pamoja na kuvamiwa na kuharikishwa (7:168)

Adhabu hizi huendelea sawa na muda Allah Alivyokadiria na Huja ghafla kama kupepesa macho bila maandalizi ya kutosha. Kila adhabu hutokea kwa sababu zake na sababu zinapobadilika ndivyo adhabu nazo huja kwa njia nyingine.

Nje ya hapo ugonjwa na adhabu zingine ni Rehema kwa mwanadamu.

Mola wetu, tumedhulumu nafsi zetu; na kama Hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara. Amin

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Mola Wetu Mtukuka

Hakika pepo yetu ni Mungu wetu na ladha yetu yote ni kwa Mola wetu. Sababu, sisi tumemwona na tumeukuta kila uzuri ndani Yake. Inafaa kujipatia hazina hii hata kwa kutoa roho. Na inafaa kununua almasi hii hata kwa kutoa uhai wote. Enyi wenye bahati ndogo kimbilieni upesi kwenye chemchem hii ambayo itatuliza kiu yenu. Ndiyo chemchem ya uzima itakayowalindeni. Nifanye nini, na niingize namna gani mioyoni mwenu maneno haya ya furaha? Kwa ngoma gani ninadi katika masoko kuwa Mola wenu ni Huyu ili watu wasikie? Na niwape tiba gani ili masikio ya watu yafunguke na yasikie?

(Roohani Khazain Jal. 19: Safina ya Nuhu Uk. 15)

MATUKIO KATIKA PICHA



Mwalimu Ally Kaisi msimamizi wa Jamaat ya Mkoa wa Pwani akimkabidhi Mkuu wa Wilaya Ndugu Christpher Ngubiagai vitabu na Kalenda ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania.



Ndg Swaleh Kitabu Pazi akimfafanulia Mkuu wa Wilaya ya Kilwa jambo katika zawadi ya vitabu alivyopewa na Jamaat ofisini kwake.



Ndg, Swaleh Kitabu Pazi akimwakilisha Amir Jamaat Tanzania kwa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Ndg, Christopher Ngubiagai wakiongea na vyombo vya habari baada ya makabidhiano hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Ndugu Christopher Ngubiagai akiongea na ujumbe wa Jamaat Ahmadiyya ofisini kwake na kutoa tathimini ya mafuriko mnamo tarehe 1 Februari, 2020.

Mafuriko ya kihistoria yaliikumba Njinjo mwishoni mwa Januari 2020 na kuacha athari kubwa. Mafuriko hayo yaliyofanya kazi ya kutisha ya kuvunja majengo mbalimbali, kusomba miti na mali za watu na hata kuchukua uhai wa viumbe wakiwemo binadamu, yaliacha msikiti wa Ahmadiyya salama salmin kati ya mitano pamoja na nyuma ya mwanajumuiya iliyokuwa pembeni mwake. Msikiti ulihifadhi baadhi ya wananchi na mali zao hadi hapo msaada ulipofika.

Watu wa Njinjo wamepata somo la aina yake juu ya kudra ya Allah kwanza kabisa kwa kuona namna mji wao wa dahari nyingi ukifutwa kuwa tambarare kwa siku chache. Kubwa ni kudhihirika kwa ukweli wa Ahmadiyya kwa kuusalimisha msikiti wa wale wanaopingwa tangu azali katika mji huo na kutimia kwa njozi za Waahmadiyya kadhaa walizoziona hapo kabla.

Habari na Mwl Ali Salum Ng'ambage, Njinjo-Kilwa



"Kujitolea ni heshima" *Rais wa Jamaat Ahmadiyya Mkoa wa Pwani akibeba viroba vya unga kuweka kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya tayari kwa ugawaji kwa waathirika wa mafuriko.*

بسم الله الرحمن الرحيم

Assalam Alaikum Warahmatullah Wabarakatuh

TAHADHARI YA UGONJWA WA CORONA (COVID 19)

Kufuatia kuzuka kwa ugonjwa wa Corona (COVID-19) Hazrat Khalifatul Masih(V)atba amekuwa akitukumbusha kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa huu sawa na mafundisho ya Islam na kusisitiza kufuata miongozo na maagizo ya Serikali na wataalam wa afya yanayotolewa ikiwa ni pamoja na;

- *Kunawa mikono kwa maji safi na sabuni.*
- *Kuepuka kupeana mikono na kukumbatiana kama ilivyozoeleka*
- *Kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima kadri inavyowezekana.*
- *Usiende Msikitini ikiwa una hali ya homa kali na mafua.*
- *Kuanzia sasa wazee, watoto na akinamama wote wasifike misikitini kwa sala za Ijumaa na nyinginezo, wasalie majumbani mwao.*
- *Madrasa zote za watoto zimesimamishwa kwa sasa hadi zitakapotangazwa tena.*
- *Maadhimisho ya Siku ya Masihi Aliyeahidiwa yamesitishwa.*
- *Mara baada ya sala watu watawanyike.*
- *Kinga pua na mdomo kwa kitambaa safi au kiwiko unapokohoa au kupiga chafya.*

Tuzidi kufanya maombi ili Allah Atunusuru na Ainusuru dunia dhidi ya madhara ya ugonjwa huu na kuendelea kuboresha hali zetu za kiroho.

Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry
Amir na Mbashiri Mkuu

Upendo wa Seyidna Ahmad[as] kwa Mtume[saw]

Kutoka uk. 10



Sheikh Karim Ud Din Shams

ni kama bahari isiyo na mipaka. Tunapata harufu za mapenzi yake kwa bwana wake kutoka katika kila neno la maandishi yake, tunaona wazi aksi ya uzuri wa Mtume[saw] kwenye mwenendo na tabia ya Seyidna Ahmad[as] tunashuhudia jazba yake ya kudumu ya kujitolea muhanga kwa heshima na taadhime ya Mtume[saw] kwenye kila nia na mpango wake.

Tangazo zuri lilioje la mapenzi na mahaba!

Ewe mpenzi wangu! Roho yangu ilishazama katika upendo wako zamani, sasa mwili wangu nao unatamani kuruka kwako, laiti ningekuwa na uwezo huu..!

Maandishi ya mtu, ndio yanayodhihirisha hisia zake za moyoni. Na maandishi ya Seyyidna Ahmad[as] kuhusu upendo wake kwa Mtume[saw] ni kama bustani ya kudumu,na yenye kutoa maua siku zote, kila ua lake limejipamba na mapenzi, mahaba, na uaminifu visivyo vya kwaida.

Nieleze maandiko yake yepi na yepi na nithubutu kuacha mengine gani? Kwani kwa hakika maandishi yake yote ni bahari ya upendo wa Mtume[saw] Ningependa kuweka mbele yenu baadhi ya mifano kutoka katika maandiko yake yaliyojaa maarifa, busara, hekima na mapenzi yasio na kifani:- Hadhrat Seyyidnaa Ahmad[as] anasema kumhusu Mtume([saw])...

"Nuru ile ya hali ya juu aliyojaaliwa mwanadamu, yaani mwanadamu mkamilifu, hawakujaaliwa malaika, wala nyota, wala mwezi, wala jua, wala haikuwemo baharini na mitoni, wala haikupatikana katika lulu, yakuti, zumaridi na almaasi .

Ilimuraadi hakuna kitu cho chote cha ardhini au mbinguni kilicho jaaliwa hiyo nuru isipokuwa mwanadamu mkamilifu, ambaye mfano wake kamili, na wa hali ya juu sana ni Mtume Muhammad[saw] aliye bwana wetu, kiongozi wetu, fahari wa manabii wote na mbora wa viumbe."

Kisha anasema: Daima nastaajabia sana Nabii huyu Mwarabu, aitwaye Muhammad, maelfu ya baraka na amani iwe juu yake. Cheo chake cha juu kilioje? Haiwezikani kujua upeo wa daraja la hali ya juu, mwanadamu hawezi kufahamu vina na undani wa athari ya khulka zake zilizotukuka. Yasikitisha daraja lake lililonyanyuka sana halikufahamika vyema. Ule umoja wa Mungu uliokuwa umetoweka duniani ukafufuliwa tena na huyu mshindi mkuu. Alimpenda Mwenyezi Mungu kwa mapenzi ya kupindukia, na kujitaabisha kwa kuwahurumia wanadamu. Ndio maana Mwenyezi Mungu, aliyemjuzi wa siri ya moyo wake, akamfadhili zaidi kuliko Manabii wote na watu wote wa zamani na wale watakaokuja baadaye, na akamtimizia matakwa ya moyo wake katika uhai wake. (Roohani Khazain Jal. 22: Hakikatul- Wahy Uk.115-116).

Tuchunguzapo kwa roho safi bila mapendeleo Manabii wote wa zamani, twapata ya kwamba Hadhrat Muhammad Mtume Mtukufu wa Islam[saw] ndiye shujaa kupita wote, ndiye aliyekusanya sifa zote za maisha na ndiye aliyempenda Mwenyezi Mungu zaidi. (Roohani Khazain Jal. 12: Siraje-e- Muneer Uk. 72)

Tunapochunguza mashairi yake, ya Kiurdu au Kiarabu au Kiajemi, tunagundua ya kwamba kila ubeti wake unadhihirisha mapenzi, mahaba na uaminifu kwa Mtume[saw] kama asemavyo, "Kila chembe cha mwili wangu kimejaa mapenzi yako, huu ndio mji tulioukalisha ndani ya moyo wetu."

Kisha katika kiajemi anasema:- "Nimejilevya kikamilifu na mapenzi ya Mtume Muhammad[saw] baada ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kama hiyo ni kufuru basi wallaahi mimi ni kafiri mkubwa sana."

Wasomaji watukufu, bila shaka yeyote ubeti huu haunamfano wake katika ulimwengu wa mapenzi na mahaba.

Mapenzi ya kweli ni kama miski isiyoweza kufichika hata mtu ajitahidi namna gani .Ulimwengu wote ni shahidi tosha wa mapenzi ya kweli aliyokuwa nayo Seyyidnaa Ahmad[as]kwa bwana wake mtukufu Muhammad[saw]. Kabla sijatoa ushuhuda wa watu ningependa kuweka mbele yenu ushuhuda wa kimbinguni ulioelezwa na Seyyidnaa Ahmad[as] Naye alisema:- Safari moja nilipata ufunuo uliokuwa na maana hii ya kwamba :- Malaika wanajadiliana katika baraza tukufu la Mwenyezi Mungu kuwa: Allah Mtukufu Anataka kumteua mtu atakayehuisha dini yake, lakini bado hajatangazwa huyu ni nani? Huzur[as] anasema muda huo huo niliwaona watu ndotoni wakimtafuta: "Muhyi" huyu, na akaja mmoja wao mbele yangu akisema kwa kudokeza kwangu, yaani huyu ndiye ampendaye zaidi Mtume[saw].

Ndugu zangu wapendwa huu ni ushuhuda uliotolewa na Mwenyezi Mungu, ambao hauna mfano wake katika historia yote ya Kiislam.

Nikitoa ushuhuda wa watu wasiokuwa Waislam, ningependa kuweka mbele yenu maneno ya Babu Muhammed Athmaan wa Lakhnau naye alisema kwamba :- Yeye alienda Qadian mnamo mwaka 1918 na kuonana na Mbaniani mmoja aitwaye Lala Malawamal au Lala Budhamal na kumuuliza kuwa unamuonaje Mirza sahib, kwani wewe ulimuona tangu umri wake mdogo ? Mbaniani huyo akajibu :-

"Sijawahi kumuona Mwislamu yeyote, mwenye kumpenda Nabii wake zaidi kuliko Mirza Sahib".

Hadhrat Dr. Mir. Mohammed Ismaail sahib akitoa ushuhuda wake wa binafsi alisema:- "Ninasema kwa kuapa kwa jina la Allah kuwa, sijamuona yeyote aliyezama katika mapenzi ya Allah na ya Mtume Muhammad[saw] zaidi kuliko Mirza Sahib".

Hadhrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad[ra] ambaye ni mwana wa pili katika watoto waliotabiriwa kuzaliwa kwa Seyidna Ahmad[a.s] ameandika:

"Najua siku moja nitakufa na kufika mbele ya Mola wangu. Basi, naapa kwa Mwumba wangu ya kuwa sikuona hata mara moja Mtume[saw] kutajwa jina lake mbele ya Seyidna Ahmad[as] ila machozi yakamlengalenga. Kila chembe cha mwili wake kilijaa mapenzi ya Mtume[saw]".

Kuna msemo wa Kiarabu usemao kwamba; "*fadhila ni ile inayoshuhudiwa na maadui pia*". Wapinzani wa Seyidna Ahmad[as] wameyatumia sana mashairi yake katika vitabu vyoa bila kutaja jina lake na hadi leo wanaendelea kufanya hivyo. Khususan mashairi na maandiko ya Seyidna Ahmad[as] yaliyojaa na mapenzi ya Mtume[saw] yameandikwa na watu wengi kwenye vitabu vyao, orodha ya majina yao ni ndefu lakini nataka kueleza mfano mmoja tu wa Maulana Jan Mohammed aliyetunga kitabu Kiitwacho, …… Mazungumzo sahih ya Kiarabu naye amenakili beti 58 za Seyidna Ahmad[as] katika kitabu hiki bila kutaja jina lake.

Sasa kama Seyidna Ahmad[as] ni kafiri mbele yao, kwanini wanaiba na kunakili mashairi yake yaliyojaa mapenzi ya Mtume[saw]

Alama moja wapo ya mapenzi ya kweli ni kwamba Aashiqi humkumbuka mpendwa wake muda wote. Seyyidna Ahmad[as] kutokana na maarifa ya kuitambua shani adhimu ya Mtume[saw] aliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, aliujaza moyo wake safi kwa mapenzi ya Mtume Muhammad[saw] kiasi hiki kwamba, alimkumbuka bwana wake usiku na mchana akimsalia na kumtakia rehema, akieleza hali yake hiyo alisema katika ubeti wake mmoja wa Kiarabu,

"kumkumbuka Mtume[saw] ni kiini cha moyo wangu na chakula cha mwili wangu ambacho ni sababu ya uhai wangu."

Pia alisema katika ubeti wa kiurdu, "Roho yangu inauhusiano imara wenye kudumu na roho ya Mtume[saw] na tumeunywesha moyo wetu kinywaji hiki cha upendo kwa wingi:"

Hadhrat Sheikh Yukub Ali Irfani Sahib anasimuliwa kuwa nilipoenda Uengereza mnamo mwaka 1925 niliwahi kuonana na Padri Dr. White Braikht ambaye aliyekuwa Missionary katika mji wa Batala naye alionana na Seyyidna Ahmad[as] mara kadhaa. Sheikh Sahib anahadihtia kuwa Padri huyu alisema: Mimi nilishuhudia jambo moja katika tabia ya Mirza Sahib, ambalo sikulipenda nalo ni kuwa: kila mara aliposingiziwa (Mtume[saw]) basi Mirza Sahib alikasirika na rangi ya uso wake ulikuwa unabadilika na kuwa mwekundu. Hadhrat Yakub Irfani Sahib alimjibu: Padre Sahib jambo linalokuchukiza ndilo linalotupendeza sisi zaidi. (unalolichukia ndilo tunalipenda)

Siku moja Seyidna Ahmad[as] alikuwa anatembeatembea peke yake uani mwa msikiti mdogo ulio jirani na nyumba yake unaoitwa Masjid Mubarak na alikuwa ananong'ona pole pole maneno fulani huku machozi yakitiririka. Wakati huo bwana mmoja kutoka nje aliingia msikitini na akamsikia akikariri ubeti wa Kiarabu uliotungwa na Hadhrat Hassan bin Thaabit r.a. wakati alipofariki Mtume[saw] nao ni hivi, " Ewe Mtume wa Mungu, wewe ulikuwa kama mboni ya macho yangu. Kwa sababu ya kufa kwako leo mimi nimepofuka. Sasa sijali anakufa nani, maana nilihofia juu yako tu na wewe umeisha ondoka dunia hii."

Sisi twajua ya kuwa Seyidna Ahmad a.s alipata mashaka mengi maishani, alipata mateso makali, aliona misiba ya jamaa wengi miongoni mwa watoto na ndugu na marafiki na alionja machungu mengi; lakini maudhi hayo yote na shida nyingi mno alizozipata hazikuweza kumfanya alie juu ya hasara zake. Ni uchungu mkubwa ulioje wa kukumbuka kifo cha Bwana wake faraghani kilichotokea miaka zaidi 1,300 uliomfanya alie machozi aliposoma utenzi wa mahaba uliotaja hasara ya kupotea kwake Mtume Muhammad[saw] duniani! katika maisha yake mtu anakabiliwa shida nyingi. Penginie anafiwa na wazazi. Pengine watoto wanakufa. Pengine mume au mke anakufa. Ni mazito sana hayo yote mwanadamu kuyavumilia. Lakini siku zinapozidi kupita majeraha hayo yanapona pole pole mpaka mtu anasahau maumivu yake. Ni makubwa yalioje mapenzi ya huyu mtumishi juu ya Bwana wake ambaye akimkumbuka msiba wake baada ya miaka 1,300, macho yake yanatiririsha machozi kama mvua kana kwamba kifo chake kimetokea leo. Jeraha la moyoni mwake halikupona ingawa zilipita karne 13.

Hapa nataka kuwaambia ndugu zangu Waislamu ambao hadi sasa

Endelea uk 11

Upendo wa Seyidna Ahmad[as] kwa Mtume[saw]

Inatoka uk 10

hawajawa na bahati ya kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya na kusaidiana nasi katika huduma ya kuuhami Uislamu ya kwamba wao wafikirie tukio hili tu peke huku wakimwogopa Mwenyezi Mungu. Je, mtu wa namna hii anaweza kutoka nje ya kundi la wafuasi wa Mtume[saw]? kisha Seyyedna[as]anasema katika shaairi lake la kiajemi kuwa:

Katika mwili wa Mtume[saw] Mwenyezi Mungu Ameweka nuru ya ajabu na chimbo lake takatifu limejaa majohari na maalmasi ya fahari, Basi enyi wenye kiburi, ikiwa mnatafuta hoja ya ukweli wake, ingieni katika wafuasi wake; maana dhati yake yenyewe ni hoja kubwa ya ukweli wake. Wallahi kama mimi nikatwe vipande vipande katika njia hii na chembe chembe zote za mwili wangu zichomwe moto na kugeuka kuwa majivu, mimi sitaondoka mlangoni pake. Ewe nafsi ya Mtume, nafsi yangu iwe sadaka kwako! Mapenzi yako yameangaza mwili wangu wote. (Aaina e Kamalat e Islam)

Katika shahiri lake jingine alilotunga kwa Kiarabu anasema akizungumza na Mtume[saw]: "Ewe Bwana wangu, nitazame kwa jicho la mapenzi na huruma, kwa sababu mimi ni mtumishi wako hakiri. Ee Mpenzi wangu, upendo wako umeninywesha moyo wangu na ubongo wangu na kila mshipa wa mwili wangu. Ee bustani ya furaha yangu, siachi kukumbuka hata kwa dakika moja. Roho yangu imekuwa mali yako na huu mwili wangu wa udongo pia watamani kuruka na kufika kwako. Laiti ningekuwa na mbawa za kuruka!" (Aina e Kamalat e Islam).

Wasomaji wapendwa! ni nani anaeweza kusahau lile tukio maarufu lililobeba ushuhuda wa malaika ambapo Seyidna Ahmad[as] aliona katika ru'uiya, malaika walileta mitungi ya nuru nyumbani kwa Seyidna Ahmad[as] na mmoja wao akisema, hizi ni baraka zako za kumsalia na kumtakia rehma Mtume[saw]

Matokeo ya lazima ya mapenzi ni mtu kutaka kujitoa mhanga nafsi yake kwa ajili ya mpendwa wake na kuwa na ghera juu yake. Haiwezekani mtu kukosa ghera kwa ajili ya mpenzi wake au kukosa nia ya kujitoa maisha yake kwa ajili yake.

Seyidna Ahmad[as] alikuwa na sifa hizi kwa ukamilifu kwa ajili ya Kiongozi wake na Bwana wake, Mtume Muhammad[saw] akitaja masingizio ya Wakristo wanayoleta juu ya nafsi takatifu ya Mtume[saw] amesema,: "Mapadre, wa Kikristo wamezua mengi juu ya Mtume wetu[saw] Hakuna kitu kilichoniudhi roho yangu zaidi kuliko hayo maneno ya dhihaka na maskhara wanayotunga wao juu ya mtakatifu Mtume wetu huyu. Moyo wangu umejeruhika kwa sababu ya hao kumkashifu na kumwaibisha mbora wa viumbe.anasema,

Haki ya Mungu, kama watoto wangu wote na wajukuu wangu na vilembwe wangu na marafiki zangu na wasaidizi wangu wote wauawe mbele ya macho yangu, hata mimi mwenyewe nikatwe mikono na miguu, na mboni za macho yangu kutolewa nje, wala nisipate mradi wangu hata moja, tena ni nyimwe furaha na starehe zangu zote shida hizi zote si kitu zikilinganishwa na msiba wa Mtume[saw] kufanyiwa mashambulio machafu. Ee Mola wetu uliye mbinguni, Utuhurumie na kusaidia na kutuokoa na mtihani huu mkubwa.

Je, ghera ya namna hii mfano wake waweza kupatikana kwa mwislamu yeyote au mahali pengine popote katika zama hizi? Je, mapenzi kama haya yaweza kuonyesha katika mtu mwingine hivi sasa? Hayo siyo madai matupu, bali kila tukio la maisha ya Seyidna Ahmad a.s liwe kubwa au ndogo, linatoa ushahidi juu ya mapenzi hayo hayo.

Safari moja Seyidna Ahmad[as] alikuwa anakula chakula nyumbani kwa baba yake mdogo. Aitwaye Mirza Ghulam Haidar Sahib, mkewe Ghulam Haidar Sahib alitamka kwa bahati mbaya neno Fulani lenye kumvujia heshima Mtume[saw] hapo Seyidna Ahmad[as]akasimama na kuondoka mara moja, bila kumaliza kula chakula chake.

Mnamo mwaka 1893 Seyidna Ahmad[as] alifanya mjadala na Wakristo wa Mji wa Amritsar, mjadala huu ulisha chapishwa kwa jina la vita tukuf….. Dr. Padri Martin Clark ambaye alikuwa mkuu wa Wakristo alimwalika Seyidna Ahmad[as] pamoja na baadhi ya Masahaba zake kwenye chai. Seyidna Ahmad[as] hakukubali mwaliko wake kwa sababu hii tu kwamba, hawa watu wanamvunjia heshima Mtume[saw] basi hatuwezi kukaa nao isipokuwa kwa ajili ya kubadilisha itikadi zao za uwongo.

Hali kadhalika, Seyidna Ahmad[as] alipofanya mjadala na Padri Deputy Abdallah Atham,siku zile zilikuwa za joto kali sana na kila mtu alikuwa anapatwa na kiuu mara kwa mara na maji ya kunywa yalikuwa yanahitajika sana na mahali pa jirani kulikuwa na kisima cha maji baridi cha Wakristo lakini Seyidna Ahmad[as] hakupenda kuchukuwa maji kutoka kwao kutokana na shutuma zao dhidi ya Mtume[saw] Tukio hili linaonesha mahaba na ghera yake kwa Mtume[saw]

Safari moja Seyidna Ahmad[as] alipokuwa kwenye mji wa Gurdaspur kwa sababu ya kesi, msimu huu ulikuwa wa joto kali zaidi basi wakati wa usiku, wafanyao huduma walitandika tandiko la Seyidna Ahmad[as] juu ya paa ya nyumba kama ilivyo ni desturi ya watu wale, ili Seyidna Ahmad[as] aweze kupumzika vizuri kwenye upepo mzuri. Seyidna Ahmad[as] alipofika juu na kuona kwamba nyumba hii haina ukuta wa pazia yaani fense wal. Basi, hakupenda kulala juu ya paa ile na aliwaambia wahudumu kuwa, mbona hamjui kwamba Mtume[saw] alikataza kulala kwenye paa ile isiyo na ukuta wa pazia juu? Hivyo Seyidna Ahmad[as] alikataa kulala huko na kushuka chini akiupitisha usiku huu ndani ya chumba kidogo, ilhali joto ilikuwa kali zaidi. Ndugu zangu! Huu ndio upendo wake kwa Mtume[saw] kwamba hakupenda kuakhirisha hata jambo ndogo.

Hadhrat Mirza Din Muhammad Sahib sahaba wake, anasimuliwa kuwa:- Seyidna Ahmad[as] alikuwa na desturi yake kwa ajili ya kuwaamsha watu wakati wa sala ya asubuhi, kwamba:- alikuwa analoga vidole vyake na maji kisha kuyarusha kwenye uso wa mtu husika, sahaba huyu anasema siku moja nilisema huzur unaweza kuniita kwa sauti ndogo kwa ajili ya kuniamsha asubuhi. Seyidna Ahmad[as] alimjibu kuwa huu ndio desturi ya bwana wangu Mtume Mtukufu[saw]

Wasikilizaji! Angalieni jinsi Seyidna Ahmad[as] anavyofuata kila nyayo ya Mtume[saw] je, mtiifu kama huyu anastahili kutajwa kafiri? Na kama huu ni ukafiri basi sisi sote pia ni makafiri makubwa.

Siku moja Seyidna Ahmad[as] alikuwa amekaa ndani ya chumba chake pamoja na Masahaba zake na wageni wengine, mtu mmoja aligonga mlango wake na sahaba mmoja alitaka kumfungulia mlango, lakini Seyidna Ahmad[as] aliharakia kwenda kwenye mlango akimwambia sahaba wake subiri subiri, ninafungua mlango mimi mwenyewe kwani wewe ni mgeni na bwana wetu Mtukufu ameagiza kwa ajili ya kumkarimu mgeni.

Kila makala aliyoandika na kila shairi alilotunga juu ya Mtume[saw] limefanana na shimo refu lenye kina kirefu lililojaa almasi na lulu za mapenzi ya mtume[saw]zisizo na kikomo.

Binti mkubwa wa Seyidna Ahmad[as] Hadhrat Nawab Mubaraka Begam, ambaye pia ni mmoja wa watoto waliotabiriwa kuzaliwa kwa Sedna Ahmad a.s ambaye ni mwenye busara nyingi na akili pevu, anasimulia hivi, "Siku moja Seyidna Ahmad[as] alikuwa hajisikii vizuri na alikuwa amelala kitandani na mama na Hadhrat Mir Nasir Nawwab (babu mzaa mama) vile vile walikuwa wamekaa karibu naye, nara yakatokea mazungumzo juu ya haji. Hadhrat Mir Nasir Nawwaab alisema ya kuwa sasa njia ya kwenda kuhiji imerahisika kidogo na ni afadhali mtu afanye haji katika siku hizi hizi. Kwa kukumbuka hivi Makka na Madina, mahali patakatifu pa Uislamu, macho ya Seyidna Ahmad[as] yakajaa machozi naye akawa anayafuta kwa kidole chake, kasha akasema, "Ni kweli na mimi pia natamani kuhiji; lakini mara nyingi hufikiri nikifika Madina, je nitaweza kujizuia nitakapotazama kaburi la Mtume[saw]?"

Wasikilizaji Watukufu!Mapenzi haya hayakuishia kwa Seyidna Ahmad[as]bali hata wafuasi wake wanakanyaga nyayo zake juu ya kumpenda mtume mtukufu[saw]ningependa kueleza mfano mmoja tu wa padre wa Afrika ya Magharibi,aliyekuwa na tabia ya kumkashifu mtume[saw] siku zote,lakini kwa fadhili za Allah alibahatika kujiunga na jumuiyya ya Ahmadiyya na imani yake iliimarika kiasi hiki kwamba alikuwa halali mpaka amsalie mtume[saw]napenda kumalizia hutuba yangu kwa maneno haya ya Seyidna Ahmad[as],Huzur anasema:

Hapana mtume wala mwombezi kwa ajili ya wanadamu,ila mtume Muhammad[saw]kwa hiyo jitahidini mumpende kwa mapenzi kweli kweli mtume huyu,mtume wa heshima na utukufu.Na wala msimheshimu mtu yeyote kuliko yeye ili mwandikiwe mbinguni miongoni mwa wale waliookoka.

Ya rabbe sale ala nabiyyeka daiman fi hazehi al.duniya wa baathin thani.

Seyyidna Ahmad[as]anasema akituelezea Baraka za kumfuata Mtume[saw]

Isingeliwezekana kwangu mimi kuipata neema hii kama nisingefuata nyayo za Bwana kiongozi wangu, fahari ya Manabii wote, Mbora wa wanadamu, Muhammad, Mteule, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake. Mafanikio yo yote nimeyapata kwa kumfuata yeye , nami najua kutokana na uzoefu uliohakiki, ya kwamba hapana awezeye kumpata Mwenyezi Mungu na kupata elimu ya ndani ya njia zake bila kumfuata Nabii huyu, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake.

Kisha anasema,

Tokio la ajabu lilitukia kwenye majangwa ya Arabia, ambapo mamia ya maelfu ya watu yakafufuka katika muda wa siku chache, na wale ambao walikuwa mafasiki kwa vizazi vingi wakava vazi la ucha- Mungu. Vipofu wakaanza kuona, na ndimi za mabubu zikaanza kububujisha elimu za kiungu. Ikatokea aina ya mapinduzi duniani ambayo hapana jicho lililokuwa kushuhudia wala sikio lililokuwa limepata kusikia mfano wake. Je, mwajua hicho kilikuwa kitu gani? Hayo yote yalisababishwa na maombi ya usiku ya mtu aliyekuwa amejipoteza kabisa kwa Mwenyezi Mungu yaliyoleta mwamko duniani na kudhihirisha maajabu yasioaminika kwamba yangeweza kuleta kwa mkono wa mnyonge yule asiyejua kusoma wala kuandika. E Mwenyezi Mungu! Mteremshie baraka zako yeye na wafuasi wake kadri ya mahangaiko na uchungu aliokuwa nao juu ya Ummah wa kiislam, na umfikishie nuru ya neema zako daima dawamu.

(Roohani Khazain Jal. 6: Barakatud Dua Uk. 10).

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jum. II - Raj. 1440 AH | MACHI 2020 | AMMAN 1399 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

"Mtume[saw] alikuwa anasema, "Pengine unalazimika kutoa sadaka, lakini hutoi, basi haramu inaangamiza mali yako ya halali. Bila shaka haramu haichanganyiki na halali ila inaihilikisha." (**Kashf-ul-Gumah**)

Serikali Yaishukuru Jamaat Ahmadiyya Kilwa

Na **Yusuf Malinda - Kibiti**

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Ndugu Christopher Ngubiagai amesema Jamaat Ahmadiyya imetoa mchango muhimu sana na wa aina yake kufuatia mafuriko makubwa yaliyoikumba Wilaya hiyo na kuonyesha azma ya Serikali kushirikiana na Jamaat Ahmadiyya hiyo kwenye maeneo mengine pia. "*Akufaae wakati wa dhiki si tu Rafiki bali ni ndugu*" alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Akipokea msaada wa vitu mbali mbali ambavyo ni Unga tani mbili na nusu na nguo zilizotolewa na wana Jamaat Ahmadiyya, Mkuu huyo alisema tatizo ni kubwa na mafuriko hayo yamebadilisha kabisa Jiografia na Maisha ya watu Njinjo na maeneo ya jirani. Mito 3 mikubwa inayopita maeneo hayo ilimepoteza muelekeo kufuatia mvua kubwa iliyonyesha milimani na maji kwenda kwenye makazi ya watu na mashamba. Hakuna kilichotoka kwani watu wamepoteza mazao na vitu vya ndani. Hali hiyo haijatokea kwa miaka sitini sasa. Familia 3714 za wakazi takribani elfu kumi na tano wameathirika na mafuriko hayo yaliyogharimu maisha ya watu ishirini na moja na wengi hawajulikani waliko, alisema Mkuu wa Wilaya kwa majonzi makubwa. Serikali kuu imetuletea helikopta ili kuwafikia waliozingirwa na maji na juhudi kubwa zinafanyika kunusuru Maisha yao. Watu kwa sasa wanaishi mashuleni kama kambi za mud ana mipango inafanywa kuwapimia viwanja kwa haraka katika maeneo salama ili Shule zifunguliwe na Maisha yarejee kama kawaida. Aliongeza Mkuu wa Wilaya.

Akitoa Msaada huo kwa niaba ya Amir Jamaat Tanzania, Ndugu Swaleh Kitabu Pazi alimueleza Mkuu wa Wilaya historia fupi ya Jamaat Ahmadiya Tanzania na Shirika lake la *Humanity First* linavyofanya kazi duniani na hapa Tanzania.

Lengo ni kuwasaidia binadamu wakati wa majanga kama haya na kutoa kile kinachowezekana kupunguza makali ya shida za watu. Msaada huu umetolewa na wanajamaat wenyewe kwa kuchangishana na hasa nguo tulizokuja nazo.

Mafuriko ni janga kubwa linambatana na maradhi na kuiomba Serikali ya Wilaya kujipanga na maradhi ya milipuko katika makambi ya muda ambayo maji safi na huduma za choo ziko duni.



Kwa niaba ya Amir Jamaat Tanzania, Ndugu Swaleh Kitabu Pazi akimkabidhi sehemu ya shehena ya vyakula na nguo Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Ndugu Christopher Ngubiagai mbele ya waandishi wa habari na kamati ya maafa ya Wilaya ya Kilwa

Amir wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry anawapa pole sana kwa janga hili na alipenda kuja mwenyewe ila kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake ametoa uwakilishi kuja kuwajulia hali na kuwakabidhi hiki kidogo tulichonacho. Alisema Ndugu Pazi.

Katika makabidhianao hayo alikuwepo Rais wa Jamaat Mkoa wa Pwani ambaye ndiye msimamizi wa Wilaya ya Kilwa kijamaat, Ndugu Yusufu Shaaban Malinda pamoja na Majlis Amila ya Mkoa huo. Aidha pia alikuwepo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ambaye ndiye Mwenyekiti wa kamati ya maafa ya Wilaya na Kamati nzima ya maafa ya Wilaya ilishuhudia makabidhiano hayo.

Ujumbe wa Jamaat Ahmadiyya ilitumia fursa hiyo kumpatia zawadi ya vitabu mbalimbali vya Jamaat kwa ajili kuvisoma kwa muda wake.

Vyombo mbalimbali vya habari vilikuwepo kwenye tukio hilo na kutoa habari kwa Watanzania wengine, Television ya ITV, TBC, Channel 10, Radio Ahmadiyya Mtwara ambayo ilirusha tukio hilo kupitia mwakilishi wake Mwalimu Abdullah Hamis Mbanga.

Ushahidi wa Kurani



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi[as]

KITABU KIPYA

Ushahidi wa Kurani

Shahaadatul-Qur'an iliandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian, India., akiijibu barua iliyotolewa na bwana mmoja jina lake Ataa Muhammad, ambaye aliuliza juu ya ushahidi wa madai ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa na endapo Waislamu hata wanawajibika kumngojea Masihi yeyote? Pia alihoji usahihi wa hadithi kwani zilikusanywa baada ya muda mrefu kupita na hadithi nyingi kuhusu Masihi Aliyeahidiwa zimeelemea kwa mpokeaji mmoja.

Ahmad a.s. alijibu kwanza kwa kueleza utegemewaji wa Hadithi ambapo funuo zinahadithiwa.

Pili, akatoa nukuu toka kwenye Quran Tukufu za mada husika. Alihitimisha kwa kuonyesha utimilifu wa bishara katika nafsi yake. Akaongezea kwamba endapo bwana Ataa Muhammad bado hajatosheka na jibu hili, atoe chapisho kusema Hilo. Kama ni hivyo, Masihi Aliyeahidiwa a.s. angeombea ishara kuonyeshwa kumhusu yeye. Bwana Ataa Muhammad hakujitokeza tena katika mjadala zaidi. Maswali yake, licha ya yote, yalimpatia Masihi Aliyeahidiwa a.s. fursa ya kulihadhiri suala hili muhimu.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba Tsh 3,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com